

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 22 Mei, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Kamili Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa mwisho wa Bunge la Kumi na Moja, Mkutano wa Kumi na Tisa, Kikao cha leo ni cha Thelathini na Tano. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. ANATROPIA L. THEONEST – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 326

Fidia kwa Wakazi wa Jimbo la Kinondoni Waliovunjiwa Nyumba

MHE. MAULID S. A. MTULIA aliuliza:-

Siku ya tarehe 17 Desemba, 2015 wakazi wa Jimbo la Kinondoni, Mtaa wa Magomeni Sunnah nyumba 690, Mtaa wa Kawawa nyumba 253, Mtaa wa Hananasifu nyumba 200, Mtaa wa Mkunguni A nyumba 51 zilivunjiwa bila wananchi kulipwa fidia.

(a) Je, ni kwa nini Serikali ilivunja nyumba za wananchi wa Jimbo la Kinondoni bila kulipa fidia?

(b) Je, ni lini Serikali itawalipa fidia na stahiki zao wananchi waliovunjiwa nyumba Kinondoni?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la ubomoaji wa vibanda na maendeleo katika Bonde la Mto Msimbazi kwa Mkoa wa Dar es Salaam lilianza tarehe 17/12/2015 na kusitishwa tarehe 22/12/2015 na kuanza tena tarehe 5/1/2016 na kusitishwa tena kupisha kesi mbalimbali zilizokuwa zimefunguliwa na mazuio mbalimbali ya mahakama. Zoezi hili lilishirikisha taasisi saba (7) za Serikali ambazo ni Ofisi ya Makamu wa Rais (NEMC); Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Idara ya Mipango Miji); Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Halmashauri

za Manispaa za DSM); Wizara ya Maliasili na Utalii (Idara ya Misitu); Jeshi la Polisi; TAKUKURU na Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ubomoaji wa vibanda katika Bonde la Mto Msimbazi lilikuwa na lengo la kunusuru maisha ya wananchi wanaoishi katika mazingira hatarishi ya Bonde la Mto Msimbazi ambao hukumbwa na maafa, upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu kila mara yatokeapo mafuriko, kupanua uwezo wa mto huo kupitisha maji ya mvua kwa kasi ili kupunguza uwezekano wa kutokea mafuriko wakati wa mvua nyingi na kuhakikisha uzingatiji wa matakwa ya sheria yanatekelezwa.

Aidha, zoezi hili liliendeshwa kwa kufuata taratibu zote za kisheria zikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa vibanda vilivyoko maeneo hatarishi; kuweka alama ya "X" kwenye nyumba zinazothibitika kuwepo katika maeneo yasiyostahili ili wahusika wahame kabla ya kubomoa; kutoa muda kwa wamiliki kubomoa wenyewe au kuhama; kuweka alama ya mpaka wa bonde; na kuondoa huduma za jamii (umeme, maji na mawasiliano).

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia, Mbunge wa Kinondoni kuwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi imeweka dawati la kupokea na kujibu malalamiko ya wananchi waathirika wa zoezi hilo. Zoezi liliendeshwa kwa haki, uwazi, bila upendeleo wala ubaguzi na watu wenye madai sahihi wamekuwa wakilipwa.

Na. 327

Stahiki za Wafanyakazi wa Kilichokuwa Kiwanda cha Sukari Kilombero

MHE. JOSEPH L. HAULE aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, zaidi ya wafanyakazi 3,000 wa kilichokuwa Kiwanda cha *Kilombero Sugar Company* walipunguzwa mwaka 2000 wakati wa kubinafsisha kiwanda

hicho kuwa chini ya mwekezaji wa *ILLOVO* na mpaka sasa bado hawajalipwa stahiki zao:-

Je, ni lini Serikali itawalipa wafanyakazi hawa mafao yao?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha *Kilombero Sugar Company* waliachishwa kazi mnamo mwaka 2000 na walilipwa stahili zao za kisheria saba zinazojumuisha, mshahara wa mwezi mmoja; malipo ya likizo; nauli za watumishi na familia zao; gharama za mizigo; mshahara wa mwezi mmoja kwa kila mwaka kwa kipindi cha miaka kumi; malimbikizo ya mishahara ambayo haikulipwa; na makato ya michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*PPF & NSSF*). Jumla ya kiasi kilicholipwa kwa wafanyakazi hao baada ya kuachishwa kazi kilikuwa ni shilingi 2,404,984,239.00.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya malipo hayo, wafanyakazi hao hawakuridhika nayo na hivyo kupelekea Serikali kufanya uhakiki wa kina wa madai hayo mwaka 2000. Taarifa ya uhakiki ilibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa jumla ya Sh.11,830,019.00 katika malipo ya awali ambazo Serikali ilizilipa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa malipo ya kisheria, wafanyakazi hao waliendelea kudai malipo ya utumishi wa muda mrefu (*Long Service Award*) yenye jumla ya shilingi bilioni 1.27 kwa madai ya kuwepo kwa Makubaliano ya Mkataba wa Hiari (*Voluntary Agreement*) kati ya Chama cha Wafanyakazi wa Kampuni hiyo (*OTTU*) na Menejimenti ya Kiwanda cha Sukari cha Kilombero madai ambayo yalikataliwa na Serikali kwa kuwa Mkataba huo haukuzingatia Sera ya Tija na Ufanisi kwani haukuweka malengo yoyote ya uzalishaji na ongezeko la tija na faida ambayo ingewezesha

kiwanda kulipa tuzo na marupurupu yaliyokusudiwa chini ya mkataba huo. Serikali inapenda kuthibitisha kwamba, malipo yote ya kisheria ya waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda cha *Kilombero Sugar Company* yalilipwa yote na hakuna madai yoyote yanayodaiwa.

Na. 328

Kampuni Iliyokuwa ya *Ultimate Security*

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, kifungu cha 56 kinaeleza kuwa ikiwa kampuni imekuwa *transferred* kwa asilimia zaidi ya 50 inatakiwa kulipa Kodi ya Ongezeko la Mtaji:-

Je, Kampuni ya *Ultimate Security* iliyouza umiliki wake kwa *Garda World*, imelipa kodi hiyo na kama imelipa ni kiasi gani?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Abdallah Majura Bulembo, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli mnamo mwezi Mei, 2019, Kampuni ya *Ultimate Security Tanzania Ltd* iliiza asilimia 5 ya hisa zake kwa Kampuni ya *M/s Garda World Holdings Cayman Ltd* ya Visiwa vya Cayman na kubadili jina la biashara na kuitwa *Garda World* jina ambalo ndilo linalotumika kwenye shughuli zote za kibiashara za kampuni hii kwa sasa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, kinamtaka muuzaji wa mali kulipa Kodi ya Ongezeko la Mtaji (*Capital Gain Tax*) pale ambapo umiliki wa mali unapofanyika. Aidha, kifungu cha 91 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 kimeweka

utaratibu pamoja na kuanisha viwango vya kodi vinavyopaswa kulipwa ambapo kwa wauzaji wazawa wanapaswa kulipa asilimia 10 ya faida kama Kodi ya Ongezeko la Mtaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mauzo hayo ya asilimia 5 ya hisa za Kampuni ya *Ultimate Security*, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilifanya makadirio ya Kodi ya Ongezeko la Mtaji (*Capital Gain Tax*) ambapo kiasi cha shilingi 9,689,793 ambayo ni sawa na asilimia 10 ya thamani halisi ya sehemu ya umiliki iliyouzwa kwa shilingi 96,897,934.30 kilikadiriwa. Kiasi hicho cha Kodi ya Ongezeko la Mtaji (*Capital Gain Tax*) kililipwa na Kampuni ya *Ultimate Security* mnamo tarehe 16 Mei, 2019.

Na.329

Watoto wa Kike wa Jamii ya Wafugaji Kunyimwa Elimu

MHE. MARTHA J. UMBULLA aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, jamii ya wafugaji nchini bado inadumisha mila na desturi potofu ya kutothamini elimu kwa watoto wa kike ambapo hunyimwa fursa ya elimu na kuozwa katika umri mdogo licha ya sheria zilizoko na maelekezo mbalimbali ya Serikali kuhusu fursa sawa kwa watoto wote kupata elimu:-

Je, ni nini kauli ya Serikali katika kupata suluhisho la kudumu na kunusuru maendeleo ya watoto wa kike kwa jamii ya wafugaji hapa nchini?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Elimu, Sura 353 na marekebisho yake ya mwaka 2016 inaeleza kuwa mtu yeyote

atakayepatikana na hatia ya kusaidia au kushawishi mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari kuolewa anaweza kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni 5, kifungo cha miaka mitano au vyote viwili kwa pamoja. Aidha, Waraka wa Elimu Na. 1 wa mwaka 2004 unaelekeza kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule waandikishwe, kuhudhuria na kumaliza elimu ya msingi kama haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa sheria na Waraka unaoelekeza masuala ya uandikishaji na mahudhurio ya lazima, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo za kutoa elimu bila malipo, kuanzisha vituo shikizi vya shule katika maeneo yenye changamoto, kujenga hosteli kwa wanafunzi wa kike na bweni kwa wanafunzi wote kwenye maeneo ya wafugaji. Aidha, ujenzi wa hosteli na mabweni unawaepusha wanafunzi wa kike kutotembea umbali mrefu wa kwenda shule na hivyo kuepuka vishawishi vinavyoipelekea kupata mimba.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu itaendelea kutoa mafunzo na elimu kuhusu madhara ya ndoa na mimba za utotoni, umuhimu wa elimu hususan kwa mtoto wa kike, stadi za maisha na malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa sharia, kanuni na taratibu zinafuatwa na kuwataka wahusika wote wanaosimamia elimu kuwabaini na kuwachukulia hatua wale wote wanaosababisha kwa namna yoyote ile mwanafunzi wa kike kukosa masomo kwa sababu ya kupata mimba au kuolewa.

Na. 330

Marejesho ya Mikopo ya Elimu ya Juu

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza:-

Kumekuwepo na ongezeko la riba na penati nyingi kwa wanufaika wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (*HESLB*) ambao wamemaliza vyuo na wanadaiwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza riba na penati hizo ili kuwanusuru waathirika?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Spika, urejeshaji na utoaji wa mikopo ya elimu ya juu unaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo, Sura 178. Kufuatia marekebisho ya sheria ya mwaka 2016, kwa sasa, sheria hii inaelekeza wanufaika wote kuanza kurejesha mikopo yao baada ya miezi 24 tangu walipohitimu masomo yao badala ya miezi 12.

Mheshimwa Spika, aidha, wanufaika ambao watapata ajira ndani ya miezi 24 baada ya kuhitimu, hivi sasa wanawajibika kuanza kurejesha mara baada ya kuajiriwa. Kwa wanufaika waliojajiri au waliopo katika sekta isiyo rasmi (*informal sector*), sheria inaelekeza kurejesha Sh.100,000 au asilimia 10 ya kipato cha mwezi wanacholipia kodi. Aidha kwa mujibu wa sheria hii, mnufaika ambaye hataanza kurejesha mkopo miezi 24 baada ya kuhitimu, adhabu yake ni malipo ya asilimia 10 juu ya deni la msingi.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na Serikali haitozwi riba (*interest*) wakati wa urejeshaji wake kama ilivyo kwa mikopo inayotolewa na taasisi za fedha za kibiashara ambazo hutoza riba kati ya asilimia 14 hadi 22. Mikopo ya elimu ya juu ya Serikali hutozwa asimilia 6 kama Tozo ya Kutunza Thamani *Value Retention Fee-VRF* ili kutunza thamani ya fedha za mkopo. Tozo hii hukatwa kwenye deni la msingi *principal loan* kadri linavyopungua na husaidia marejesho kuwa na thamani ya

kuweza kutumika kuwakopesha Watanzania wengine wahitaji.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wanufaika wote wa mikopo ya elimu ya juu kujitokeza kwa wakati na kuanza kurejesha mikopo. Aidha, nawakumbusha waajiri kuhakikisha makato yote kutoka kwa wanufaika yanawasilishwa kwa Bodi ya Mikopo ndani ya siku 15 baada ya kila mwisho wa mwezi kama inavyoelekezwa na sheria.

Na.331

Hitaji la Maji – Jimbo la Geita Vijijini

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Jimbo la Geita Vijijini limezungukwa na Ziwa Victoria lakini Jimbo hilo halina mradi wa maji. kuna mradi mmoja katika Kijiji cha Mharamba, Kata ya Nkome ambao umetumia zaidi ya 1.51 lakini hautoi maji toka ulipokamilika mwaka 2015 kutokana na kuchakachuliwa.

Je, ni lini Serikali itatembelea mradi huo ili kujionea wizi huo na kutupatia mradi mwingine utakaowanufaisha wananchi?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Jimbo la Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji ya bomba katika Kijiji cha Mharamba ambao ulitekelezwa kwa gharama ya Sh.1,255,247,672.08 ulianza kutekelezwa tarehe 30 Januari, 2013 na kukamilika na kuanza kutoa huduma tarehe 30 Mei, 2015. Mnamo Desemba, 2019 transfoma inayopeleka umeme kwenye mradi iliungua hali iliyosababisha mradi kusimama kutoa huduma. Serikali kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* ilifanya jitihada za kurejesha huduma ya maji kwa wananchi

mapema lakini mvua zilizokuwa zinanyesha zilipelekea kazi hiyo kuchelewa kukamilika kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, kwa sasa huduma ya maji imerejeshwa baada ya tatizo hilo kufanyiwa kazi na watu waishio katika kijiji hicho wanaendelea kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo la maji lililopo katika Jimbo la Geita Vijijini, Serikali itatekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mjini Geita utakaonufaisha watu wapatao 615,741 waishio katika Mji wa Geita na vijiji 18 vilivyopo katika Jimbo la Geita Vijijini ambavyo ni Kasota, Nyabalasana, Kakubilo, Kikwete, Luhala, Buligi, Senga, Kaseni, Chanika, Buhangizi, Lwemo, Kagu, Nyamigana, Kibwela, Nyawilimilwa, Ntanchi, Bugulula na Nyansalwa. Mradi huu ambao utatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya India unategemewa kuanza mapema Agosti, 2020.

Na.332

Mradi wa Maji Bwawa la Kawa, Isale na Mpsa

MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-

Miradi ya Maji ya Bwawa la Kawa, Isale, Mpsa na Kijiji cha Kisula imegharimu Serikali zaidi ya shilingi bilioni 3 mpaka sasa, lakini miradi yote haitoi maji. Waziri na Naibu Waziri wa Maji wametembelea mara 2 miradi hii lakini mpaka sasa haitoi maji na mingine haijakamilika.

Je, ni lini miradi hiyo itakamilika na kutoa huduma ya maji kwa wananchi?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ujenzi wa Bwawa la Kawa umekamilika na Bwawa hilo linahudumia vijiji vya

Kalundi, Nkundi na Fyengeleza. Hata hivyo, kipindi cha masika chenye mvua nyingi kuanzia Novemba 2019 hadi sasa kumekuwa na tatizo la kujaa kwa tope zito mara kwa mara kwenye kisima cha kuchukulia maji (*sump well*) na hivyo uzalishaji wa maji kushindikana. Baada ya mvua kuisha kazi ya ujenzi itaanza ili kuzuia tope na mmomonyoko kwenye chanzo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Isale umefikia asilimia 65 ambapo ujenzi wa banio umekamilika. Mkandarasi wa mradi huu amefutiwa usajili na Bodi ya Wakandarasi kuanzia Oktoba 2019. Kazi zilizobaki zimefanyiwa tathmini ambapo zitafanyika kwa *Force Account*. Tayari Serikali imetuma shilingi milioni 200 katika ofisi ya RUWASA Mkoa wa Rukwa ili kuendelea na utekelezaji wa mradi huo. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika ifikapo Sptemba 2020. Mradi wa Kisula umefikia asilimia 70. Kazi zinazoendelea kukamilishwa ni pamoja na ufungaji wa umeme, pampu na ulazaji wa bomba lenye urefu wa mita 960 ili wananchi waanze kupata huduma ya Maji.

Na. 333

Tatizo la Mawasiliano Chunya

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Kijiji cha Sipa, Kata ya Kambikatoto, Wilayani Chunya kina wakazi zaidi ya elfu kumi (10,000) lakini kuna shida kubwa ya mawasiliano.

Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya mawasiliano katika kijiji hicho?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za mawasiliano nchi nzima. Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulitangaza zabuni ya Awamu ya Pili B, Januari 2015 ambapo Kata ya Kambikatoto ilijengwa minara miwili ambayo ni Kambikatoto Site 1 na Kambikatoto Site 2. Aidha, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unafanya tathmini katika kata hiyo ili kubaini maeneo yasiyo na mawasiliano au yenye mawasiliano hafifu kwa ajili ya kuboresha huduma za mawasiliano ili wananchi waweze kuwasiliana kwa urahisi.

Na. 334

Barabara ya Ifakara – Mlimba - Madeke – Njombe

MHE. SUSAN L. KIWANGA aliuliza:-

Barabara ya Ifakara – Mlimba, Mlimba – Madeke - Njombe ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Mlimba na Njombe.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa kuwa upembuzi yakinifu umeshafanyika?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ifakara – Mlimba – Taweta – Madeke yenye urefu wa kilomita 220.22 ni barabara ya Mkoa yenye kiwango cha changarawe na udongo inayounganisha mikoa ya Morogoro na Njombe katika Kijiji cha Madeke. Sehemu kubwa ya barabara hii inapitika vizuri wakati wote wa mwaka, isipokuwa maeneo machache yanayohitaji kuimarishwa ili nayo yapitike wakati wote wa

mwaka. Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Serikali inaendelea kuimarisha maeneo korofi kila mwaka kadri fedha inavyopatikana ili hatimaye barabara yote ipitike bila shida.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshakamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara kutoka Ifakara hadi Kihansi (kilometa 126) ili kuunganisha na kipande cha barabara ya lami (kilometa 24) kilichoingwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba.

Aidha, kwa upande wa Mkoa wa Njombe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Kibena – Lupembe – Madeke (kilometa 123) umekamilika. Upembuzi yakinifu wa kina na usanifu wa kina wa sehemu ya Kihansi – Taweta – Madeke (kilometa 100) umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) chini ya mradi wa Mkange – Tungamaa – Pangani. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Ifakara hadi Kihansi (kilometa 126) ambayo usanifu umekamilika.

Na. 335

Ndoa za Utotoni Nchini

MHE. ESTER A. MAHAWE aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa ndoa za utotoni hali inayoathiri watoto kisaikolojia na makuzi.

Je, ni lini Serikali italeta marekebisho ya sheria hii ili kunusuru maisha ya watoto wetu wa kike?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Spika, awali ya yote, napenda kueleza kuwa si sahihi kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa ndoa za utotoni. Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na matatizo ya ndoa za utotoni. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka masharti ya uwepo wa ridhaa ya wazazi au Mahakama hususan kwa mtu anayetaka kuolewa chini ya umri wa miaka 18 kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, aidha, Sheria ya Elimu, Sura ya 353 imeweka katazo kwa mtoto wa kike aliye katika elimu ya msingi na sekondari kuolewa na endapo hili linatokea, basi mtu aliyeoa mwanafunzi atashtakiwa kwa kubaka na wazazi waliohusika pia watachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimwa Spika, kutokana na Sheria ya Ndoa, 1971 kutungwa baada ya maridhiano na wadau mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya dini, mila, desturi na tamaduni za Mtanzania, marekebisho ya sheria hiyo yanahitaji mjadala wa kutosha ambao unahitaji kuridhiwa bila kuleta migogoro katika jamii. Pamoja na hayo na kwa kuwa hatua za kumlinda mtoto wa kike zimechukuliwa kupitia sheria mbalimbali, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu athari za ndoa za utotoni na kutekeleza sheria zilizopo wakati mjadala kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ndoa unaendelea.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH -KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2019

SPIKA: Ahsante sana Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoyua kwamba Bunge hili la mwisho na tusingependa Bunge hili la Kumi na Moja likaacha kiporo kwa Bunge la Kumi na Mbili. Tumekubaliana katika Kamati ya Uongozi kwamba ni vizuri *homework* zetu zote zikamilike mojawapo ilikuwa ni kupata taarifa za Kamati za Kudumu za Hesabu. Kwa hiyo, tutakuwa na kamati ya Hesabu za Serikali leo na siku ya Jumanne na itafuatiwa na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa siku mbili tena Jumatano na Alhamisi ya wiki ijayo.

Kwa jinsi hiyo basi, moja kwa moja nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Kaboyoka au mwakilishi wake. Karibu sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Aeshi.

MHE. KHALFANI H. AESHI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(17) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kuhusu taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na *CAG* za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2019 na kuomba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Kamati za Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za jumla ya mafungu 17 ya Serikali Kuu na mafungu 20 ya Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya *CAG* kwa mafungu mahususi (Serikali Kuu na Mashirika ya Umma) ulibainisha hoja za mafungu 15 kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, hoja namba moja, tathmini na ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Kwa kipindi cha miaka 5 toka mwaka 2015 hadi 2020,

TRA imeongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kisheria ambapo kati ya mwaka 2016 hadi 2019, *TRA* ilifanikiwa kukusanya mapato kwa wastani wa asilimia 88.1 kilinganishwa na malengo ambayo wamekuwa wakipewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya *CAG* umebaini changamoto katika maeneo yafuatayo:-

(a) Katika Idara ya Ushuru wa Forodha, Kamati imebaini hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 kiasi cha fedha cha shilingi bilioni 712.4 kilikuwa hakijakusanywa kutokana na dosari mbalimbali.

(b) Jumla ya mashauri ya kodi yenye thamani ya shilingi bilioni 84.6 yalikuwa hayajahitimishwa. Hali hii kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na vyombo vinavyohusika na utoaji wa maamuzi ya kodi *TRAB* na *TRET* kutokutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali.

(c) Changamoto za ukusanyaji wa madeni ya kodi ya siku za nyuma (*tax arrears*) kiasi cha shilingi bilioni 303.

Mheshimiwa Spika, hoja namba mbili, madeni ambayo *TANESCO* inada'i kwa Taasisi za Serikali na kwa wateja binafsi yenye thamani ya shilingi bilioni 454.4. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019, Shirika la Umeme *TANESCO* lilikuwa linada'i jumla shilingi bilioni 454.4 kutoka kwa wateja mbalimbali. Mchanganuo wa deni hilo unafafanua kwamba Taasisi mbalimbali za Kiserikali zinazodaiwa jumla ya shilingi bilioni 205.8 na wateja binafsi shilingi bilioni 199.3 na madeni mengineyo jumla yake ni shilingi bilioni 49. Athari ya uwepo wa deni lילוambatanishwa katika chati namba 2.1 hapo juu ni kupungua kwa hali ya ukwasi *liquidity* ya *TANESCO* na hivyo kuathiri hali ya kiutendaji wa shirika hilo muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tatu, usimamizi wa mkataba na hali ya ufanisi katika Mamlaka ya Bandari (*TPA*). Pamoja na mafanikio ambayo *TPA* imepata ikiwa ni pamoja

na ongezeko la shehena za mizigo inayoainishwa katika chati namba 2.2, taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa changamoto kadhaa ambazo zinapunguza ufanisi wa shirika hilo. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Upungufu katika mfumo wa makusanyo ya fedha ya bandari (*TPA Billing System*). Upungufu huo unasababisha dosari kadhaa ikiwemo uwepo wa shilingi bilioni 2 ambazo ni tofauti ya fedha ambayo haikuwa imefanyiwa usuluhishi na hati za madai za shilingi bilioni 1.8 ambazo hazikuonekana.

(b) Dosari katika usimamizi wa mikataba ambapo katika mikataba saba iliyokaguliwa CAG alibaini kutokuwepo taarifa za maendeleo ya miradi (*Project Progress Report*).

(c) Ongezeko la deni ambalo TPA inadai kwa wateja kwa mwaka 2019 ambapo kwa bandari ya Dar es Salaam ilikuwa ni shilingi bilioni 25. Hii ni kinyume na kifungu namba 3.3.3 cha Kanuni za Fedha za TPA ambazo kinataka huduma zote za bandari zilipwe kwa fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, hoja namba nne, matumizi yasiyo na manufaa ya shilingi bilioni 1 kwa Wakala wa Umeme (*REA*). Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG umebaini kuwa REA waliingia mkataba na Kampuni ya *SMEC International Limited* kwa ajili ya shughuli za ushauri wa kitaalamu. Shughuli hizo zilihusu uandaaji wa nyaraka za sabuni (*Bid Documents*) kwa ajili ya ushauri na usanifu wa kina wa ujenzi wa njia ya mkondo wa kati wa umeme yaani *Medium Voltage* kwa ajili ya vijiji 7,893 hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kabla kampuni husika hajjakamilisha taratibu za ushauri, REA na TANESCO waliteua wakandarasi 29 waanze kutekeleza mradi husika. Kwa msingi huo, Kampuni ya *SMEC International Limited* ililipwa fedha kwa kuandaa taarifa ambayo REA na TANESCO hawakuitumia katika utoaji wa zabuni kwa wakandarasi husika.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tano, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*). Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ya *CAG* kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*), umebaini upungufu katika maeneo makubwa mawili. Maeneo yenye dosari ni katika utunzaji wa malighafi za uzalishaji vitambulisho vya Taifa zenye thamani ya shilingi bilioni 42; na eneo la pili ni kutokuwepo kwa mkataba kati ya *NIDA* na watumiaji wa taarifa za *NIDA* hivyo kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, hoja namba sita, matokeo ya ukaguzi maalum kuhusu mali na madeni ya Kampuni ya PRIDE. Kwa muhtsari *CAG* alibaini yafuatayo katika kampuni ya Pride.

(a) Jumla ya shilingi bilioni 11.1 madeni yaliyochukuliwa na watumishi wapatao 201 bila kurejesha hadi kufikia tarehe 30 Oktoba, 2019.

(a) Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2019 Kampuni ya PRIDE inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 130.

(c) Ukaguzi maalum ulibaini ubadhirifu wa fedha uliofanywa na baadhi ya watumishi wa Kampuni ya PRIDE kiasi cha shilingi bilioni 10.4.

(d) Ubadhirifu wa fedha za malipo ya watoa huduma mbalimbali kwa huduma ambazo hazikufanyika kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017 shilingi milioni 585.9.

Mheshimiwa Spika, hoja namba saba, matumizi ya shilingi bilioni 1.51, Wizara ya Maliasili na Utalii bila kuwepo kwenye mpango wa bajeti. Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, kama zilivyorekebishwa mwaka 2014 zinalipa Bunge mamlaka ya kupitisha na kuridhia matumizi yoyote ya fedha za Serikali. Taarifa ya *CAG* inabainisha kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ilikusanya fedha kutoka taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hiyo kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya shughuli ya Tamasha la Utalii (*Utalii Festival*). Hata hivyo, ukaguzi unabainisha kuwa fedha hizo

zilitumika bila idhini ya Bunge kama Kanuni za Fedha za Umma zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, hoja namba nane, ni hali ya kifedha ya benki zinazomiliki na Serikali. Uchambuzi wa Kamati katika mwenendo wa Benki za Serikali katika mwaka wa fedha 2019 ulibaini kuwa Benki ya Uwekezaji Biashara na Benki ya Uwekezaji Maendeleo zina changamoto kubwa ya mtaji. Hali hiyo inatatiza utendaji wenye ufanisi na malengo ya kuanzishwa Benki hizo. Kutokana na changamoto za mtaji, Benki ya Uwekezaji Maendeleo na Benki ya Uwekezaji Biashara zinaweza kupewa adhabu na Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) na hata kufungiwa leseni ya biashara kwa kukiuka miongozo muhimu inayosimamia shughuli za benki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tisa, kutofanyika tathmini ya uwezo (*actuarial valuation*) wa Mfuko wa *PSSSF*. Baada ya kuunganishwa kwa mifuko mbalimbali ya jamii na kuwa *PSSSF*, *CAG* alitoa mapendekezo kuwa ni muhimu kufanyika tathmini ya kitaalamu na kutambua uwezo wa Mfuko wa *PSSSF* kuweza kutimiza majukumu yake na kulipa *pension* kwa siku zijazo. Zoezi hili hufahamika kitaalamu kama *actuarial valuation*.

Mheshimiwa Spika, hadi ukaguzi wa mwaka 2019 unamilika zoezi hili la tathmini lilikuwa halijakamilika. Athari ya kutokufanyika kwa zoezi hilo muhimu ni kwamba mfuko utakosa tathmini ya kina iwapo una uwezo wa kulipa mafao siku zijazo kwa kutumia rasilimali ulizonazo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi, kutokusainiwa kwa hesabu za Shirika la Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) baada ya kutolewa hati isiyoridhisha (*qualified audit opinion*). Ukaguzi wa Hesabu za Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*) ulikamilika mnamo mwezi Desemba 2019. Katika ukaguzi huo, *CAG* alitoa Hati Isiyoridhisha (*Qualified Audit Opinion*) kwa hesabu za *TTCL*. Hata hivyo, kinyume na masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Na. 11 ya Mwaka 2008 Bodi ya *TTCL* haikupokea na kuridhia taarifa husika ya

ukaguzi iliyokuwa na hati iliyopendekezwa ili baadaye isainiwe na CAG.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya *TTCL* kutokupokea na kuridhia taarifa ya ukaguzi kwa wakati kwa sababu ya hoja zilizomo na hati ya ukaguzi iliyopendekezwa ni hali ya kuingilia uhuru wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*NAOT*). Aidha, *CAG* alibaini uwepo wa kiasi cha shilingi bilioni 11.1 ambazo ilionekana kuwa ni deni ambalo *TTCL* inadaiwa na wateja wake bila uthibitisho na kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho wa deni la shilingi bilioni 91.43 ambalo *TTCL* inadai kwa wateja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na moja, kutolewa Hati Mbaya ya Ukaguzi (*Adverse Opinion*) kwa Kampuni ya *STAMIGOLD*. Kwa mwaka wa ukaguzi 2018/2019, Kampuni ya *STAMIGOLD* ilipata Hati Mbaya ya Ukaguzi (*Adverse Opinion*). Kampuni ya *Stamigold* ilipata Hati Mbaya ya Ukaguzi kutokana na masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Kutokuwepo kwa uthibitisho wa deni la jumla ya shilingi bilioni 52.5 ambalo Kampuni ya *Stamigold* inadaiwa; na

(b) Kutokuwepo kwa uthibitisho wa deni la jumla shilingi bilioni 52.5 ambalo Kampuni ya *Stamigold* inadai kwa makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na mbili, matumizi ya Bodi za Mazao kuzidi mapato hivyo kutofikiwa kwa malengo. Changamoto kubwa ambayo *CAG* ameibanisha katika Bodi za Mazao ni matumizi makubwa ya bodi hizo kuliko uwezo wake. Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018/2019 ulibaini kati ya Bodi za Mazao tisa, bodi tano sawa na asilimia 56 zilikuwa na nakisi kwenye mwaka huo hivyo kuathiri utendaji wa kazi wa bodi hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na tatu, Kampuni ya *Mkulanzi* inayomilikiwa na *Mfuko wa Taifa wa*

Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa asilimia 96 na Jeshi la Magereza kwa asilimia 4. Kutokana na taarifa ya upembuzi yakinifu ya mwezi Januari, 2019, *CAG* alibaini kuwa kampuni ilipaswa ianze uzalishaji wa sukari katika kipindi cha mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi *CAG* anakamilisha ukaguzi Desemba 2019, kampuni ilikuwa haijaanzisha uzalishaji. Hali hii inapelekea kampuni kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019, kampuni ilikuwa imepata hasara ya jumla ya shilingi bilioni 8.87 sawa na asilimia 30 ya kiasi kilichowekezwa.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na nne, Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*). Kamati imebaini kuwa *BoT* inachukua muda mrefu kuhesabu fedha zinazotoka kwenye mabanki ya kibishara. Hadi ukaguzi unakamilika *CAG* alibaini zaidi ya shilingi bilioni 300 zilikuwa zinahusika katika hoja hii. Taarifa ya *CAG* inabainisha pia *BoT* inachukua muda mrefu katika kuharibu fedha chakavu zinazotoka kwenye mzunguko.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na tano ambayo ni ya mwisho, kutokuwepo na ufanisi katika kampuni ya Mzinga. Pamoja na kuwa kampuni hii imekuwepo kwa miaka takribani 10, *CAG* amebaini mapungufu mbalimbali katika uendeshaji wake ikiwa ni pamoja na kupata hasara mfululizo na pia kampuni haina Bodi ya Wakurugenzi hadi sasa kinyume na masharti ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati, Mamlaka ya Mapato (*TRA*). Ili kuongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi, Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali iboreshe hali ya utendaji wa vyombo vinavyotoa maamuzi kuhusu mashauri ya kodi kwa kutenga na kutoa fedha na rasilimali nyingine kwa wakati na kuwezesha uhitimishaji wa mashauri ya kodi kwa wakati. (*Makofi*)

(b) Serikali iwezeshe *TRA* kuwa na uwezo wa kushughulikia mashauri ya kikodi na ukusanyaji wa madeni na kodi zilizokadiriwa. Jambo hili litafanikiwa kwa kutenga na kutoa rasilimali za kutosha, uwepo wa watumishi wenye ueledi na sifa katika Kitengo cha Ukaguzi wa Kodi, Kitengo cha Huduma za Kitaalamu na Idara ya Usimamizi wa Madeni ya Kodi.

(c) Serikali iimarishe mfumo wa udhibiti katika huduma ya utoaji mizigo na ulipaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingizwa ndani ya nchi kwa kuhakikisha huduma zote za forodha zinafuatwa ipasavyo ili kuepuka upotevu wa mapato.

(d) Serikali iimarishe udhibiti na ufuatiliaji wa mizigo inayopitia hapa nchini kwenda nchi za nje (*transit goods*) ili kuepuka matumizi ya bidhaa hizo katika soko la ndani bila kulipiwa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, azimio namba mbili, malipo yasiyo na manufaa yaliyofanywa na *REA*. Bunge liazimie kwamba Serikali ifanye uchunguzi wa kina kuhusu malipo hayo ambayo yana viashiria vya ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, azimio namba tatu, usimamizi wa mikataba na ufanisi wa Mamlaka ya Bandari (*TPA*). Bunge linaazimia kwamba *TPA* itekeleze kwa ukamilifu matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake katika eneo la usimamizi wa mikataba.

Mheshimiwa Spika, pia *CAG* kwa mamlaka yake ya kikatiba na kisheria aendelee na zoezi la Ukaguzi Maalum katika eneo la manunuzi, usimamizi na utendaji na mifumo mbalimbali ya *TPA*. Aidha, Serikali izingatie mapendekezo ya Ukaguzi huo Maalum pindi utakapokuwa imekamilika ili kuboresha shughuli za *TPA*.

Mheshimiwa Spika, azimio namba nne, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*). Bunge liazimie kwamba *NIDA* iimarishe udhibiti wa ndani kwa kuwa na kumbukumbu sahihi

za mahitaji halisi na malighafi ili kufanya manunuzi kwa kuzingatia mahitaji halisi kwa kipindi kifupi. Mbili, *NIDA* iingie mkataba na taasisi zote zinazotumia taarifa za *NIDA* ili kuongeza mapato ya Serikali na kudhibiti taarifa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, azimio namba tano, madeni ya Shirika la Umeme (*TANESCO*). Bunge liazimie kwamba *management* ya *TANESCO* iimarisha mikakati ya ukusanyaji wa madeni ili kuhakikisha madeni husika yanakusanywa kwa wakati. Mbili, Serikali ichukue jitihada mahsusi za kibajeti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinazodaiwa na *TANESCO* zinalipa madeni yao kwa kuzingatia utaratibu wa kibajeti utakaokuwa umewekwa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, azimio namba sita, Ukaguzi Maalum wa Kampuni ya *PRIDE Tanzania*. Bunge liazimie kwamba Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na *CAG* katika Ukaguzi Maalum wa Kampuni ya *PRIDE* ili kuendelea kuimarisha udhibiti na uwajibikaji katika fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, azimio namba saba, matumizi ya Sh.1,511,995,000.98 katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Bunge liazime kwamba *CAG* kwa mamlaka yake ya kikatiba na kisheria aendelee na Ukaguzi Maalum anaofanya kuhusu utaratibu uliotumika kukusanya fedha hizo, matumizi yake na tathmini ya faida iliyopatikana kwa matumizi husika.

Mheshimiwa Spika, azimio namba nane, hali ya kifedha ya benki za Serikali. Bunge liazimie kwamba Serikali ifanye tathmini ya mwenendo wa benki hizo mbili; Benki ya Uwekezaji Biashara na Benki ya Uwekezaji Maendeleo, ipitie na kuchambua kwa kina viwango vya mitaji kwa malengo ya kuziongezea mtaji ili ufikie uwiano wa kiwango cha chini cha mitaji kinachotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Benki za mwaka 2014 au kuzirekebisha kwa kadri itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, azimio namba tisa, tathmini ya hali halisi ya Mfuko wa *PSSSF*. Bunge liazimie kwamba Bodi ya *PSSSF*

ihakikishe kabla ya kufikia Septemba 2020 zoezi hili muhimu liwe limekamilika.

Mheshimiwa Spika, azimio namba kumi, Kampuni ya *Mzinga Holding Company Limited*. Bunge liazimie kwamba Shirika la Mzinga lifanye mapitio ya mpango mkakati wake ili kutathmini iwapo Kampuni tanzu ya *Mzinga Holding Company* itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa muundo wa sasa au livunjwe na kuunganishwa na shirika mama kwani shughuli zao zinashabihiana. Hii itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na kwa kuunganisha nguvu ufanisi utaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, azimio namba kumi na moja, Kampuni ya *STAMIGOLD*. Bunge liazimie kwamba Serikali kupitia Wizara ya Madini itekeleze yafuatayo:-

(a) Bodi na *Management* ya *STAMIGOLD* wahakikishe wanawasilisha kwa *CAG* nyaraka zote zinazotakiwa ili uhakiki ufanyike kuhusu madeni mbalimbali ya kampuni.

(b) Serikali kupitia TAKUKURU wakamilishe kwa wakati uchunguzi wa tuhuma mbalimbali unaoendelea katika Kampuni ya *STAMIGOLD* kwa haraka na kuchukua hatua stahiki; na

(c) Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina wahakikishe Kampuni ya *STAMIGOLD* inapata rasilimali za kutosha kama watumishi wenye sifa, weledi na wabunifu. Aidha, mtaji wa Kampuni ya *STAMIGOLD* uongezwe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa kwa siku zijazo kampuni hii inasajiliwa katika Soko la Hisa Dar es Salaam ili Watanzania wapate fursa ya kumiliki hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, azimio namba kumbi na mbili, hali ya ukwasi katika Bodi ya Mazao hapa nchini. Bunge liazimie kwamba Wizara ya Kilimo ifanye tathmini ya kina na kitaalam ili kubaini faida na hasara za uwepo wa bodi nyingi za mazao. Tathmini hiyo isaidie kuangalia uwezekano wa kupunguza baadhi ya bodi kama uwezo wa kuziendesha haupo ili kuwe

na bodi chache zenye majukumu mchanganyiko na zipewe rasilimali ya kutosha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, azimio namba kumi na tatu, Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*). Bunge liazimie kwamba *BoT* iandae mpango mkakati wa muda mrefu na kurekebisha dosari za kuchelewa kuhesabu fedha zinazotoka kwenye mabenki ya biashara mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, azimio namba kumi na nne; Bunge liazimie kwamba Kampuni ya *Mkulazi Holding* itekeleze majukumu yake kwa mujibu wa mpango mkakati wa kampuni. Aidha, Serikali kupitia *NSSF* ifanye uchambuzi wa tathmini ya kina kuhusu mradi huo ili kupata njia bora ya kutekeleza bila kupata hasara na kwa maslahi mapana ya taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, azimio namba kumi na tano, kutosainiwa kwa hesabu za *TTCL* na dosari za kiutendaji katika kampuni hiyo. Bunge liazimie kwamba Serikali ifanye tathmini ya kina ya kiutendaji ya Bodi na Menejimenti ya *TTCL*. Kwa kufanya hivyo, Serikali itabaini maeneo ya kuboresha ili kampuni hiyo iendeshe katika misingi ya utawala bora, ubunifu na ushindani na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati ya *PAC* katika kipindi hiki cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja. Napenda kutumia fursa hii adhimu kwa umuhimu wa kipekee kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao kwa miaka hii mitano umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti pale Kamati inapohitaji msaada wako. Aidha, namshukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusaidia kuongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa uadilifu na weledi mkubwa. Wajumbe hawa kwa kipindi hiki cha miaka mitano

wamefanya kazi kubwa bila kuangalia misimamo ya vyama na kwa wakati wote waliongozwa na weledi, uzalendo, umoja na maslahi mapana ya taifa letu. Nawatakiwa kila la kheri katika mchakato wa uchaguzi unaokuja. Naomba majina yao yaingie kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kupitia kwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara hiyo Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Ndugu Wilfred Magova.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati inatambua na kutathmini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka kwa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu Charles Kichere na shukrani kwa uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuendelea kuisaidia Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake kwa weledi na ufanisi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA
SERIKALI (PAC) KUHUSU TAARIFA YA CAG KWA HESABU
ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA
KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2019
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (17) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (17) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba

kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mwaka 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Spika, Kwa muktadha huo, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

1.2 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

1.3 Masuala yaliyozingatiwa katika utekelezaji wa shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2020, zililenga kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2019. Kwa msingi huo, mafungu yaliyopitiwa na kujadiliwa na Kamati yalichaguliwa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: -

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Wizara, Idara, Wakala, Balizi au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;

c) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa fungu husika;

d) Hoja za ukaguzi za siku za nyuma ambazo hazijatekelezwa kikamilifu katika mafungu husika na ambazo zinahitaji ufuatiliaji wa karibu wa Kamati;

e) Kipaumbele kwa sekta na mashirika mkakati (*Strategic sectors and parastatals*) kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya sasa ya Serikali; na

f) Kipaumbele kwa kaguzi maalum (*Special audit*) zilizofanyika hivi karibuni.

1.4 Njia zilizotumiwa na Kamati katika kutekeleza majukumu yake

Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kuongeza ufanisi katika shughuli za Kamati, Kamati ilitumia njia zifuatazo katika kutekeleza majukumu yake: -

a) Uchambuzi wa taarifa za ukaguzi za fedha (*Individual financial audit reports*) za mafungu mbalimbali;

b) Uchambuzi wa matumizi ya fedha (*Expenditure*) katika mafungu ili kubaini iwapo fedha zilitumika kama Bunge lilivyoidhinisha;

c) Uchambuzi wa matumizi ya fedha ili kubaini iwapo matumizi hayo yalifanyika kwa kuzingatia misingi ya ufanisi, uwekevu na taratibu zilizopo;

d) Mahojiano na Maafisa Masuuli mbalimbali na Wenyevidi wa Bodi za Mashirika ya Umma kuhusu hoja za ukaguzi katika mafungu yao;

e) Uchambuzi wa barua ya hoja za ukaguzi kwa Menejimenti (*Management letter*) ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kama yalivyotolewa na CAG; na

f) Kufanya tathmini iwapo Serikali ina mikakati ya udhibiti wa ndani katika matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na uwepo wa mfumo wa kujipima katika ufanisi wa matumizi ya fedha. Eneo hili Kamati ilifanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani iliyopo katika mafungu yaliyokaguliwa.

1.5 Muhtasari wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2019 Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alifanya ¹ukaguzi wa jumla ya Taasisi 296 za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara zinazojitegemea, Wakala, Mifuko

¹ Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977


maalum, Sekretarieti za Mikoa, Vyama vya Siasa, Bodi za Mabonde ya Maji na Balazi. Ukaguzi ulihusisha pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa (*Consolidated accounts*), ukaguzi wa malipo tarajali ya pensheni na kaguzi maalum.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Mashirika ya Umma, Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikaguzwa na kutoa Taarifa ya Jumla ya Mashirika ya Umma 148 ikilinganishwa na Mashirika ya Umma 122 yaliyokaguliwa kwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za jumla ya mafungu 17 ya Serikali Kuu na mafungu 20 ya Mashirika ya Umma. Katika kufikia idadi husika ya mafungu, Kamati ilitumia vigezo vilivyoainishwa katika aya namba 1.3 ya taarifa hii kuchagua mafungu ya kujadiliwa. Ilikuwa ni jambo la muhimu kuchagua mafungu machache (*Sampling*) lakini yenye hoja za msingi ili kutoa ushauri kwa Serikali. Kwa baadhi ya mafungu, Kamati ilitumia taarifa ya CAG kufanya rejea kwa hoja za ukaguzi na kisha kutumia taarifa za uhakiki za CAG kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa mafungu yaliyojadiliwa na Kamati kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019 umefafanuliwa katika chati Namba 1.1 hapa chini: -

Chati Na. 1.1: Mafungu yaliyojadiliwa na Kamati kwa mwaka 2020



Chanzo: Uchambuzi wa Kamati kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka 2020

Mheshimiwa Spika, Kama chati Na. 1.1 inavyofafanua, Jumla ya mafungu 17 ya Serikali Kuu sawa na asilimia 46 yalipitiwa na kujadiliwa na Kamati. Aidha, mafungu 20 ya mashirika ya umma sawa na asilimia 54 pia yalipitiwa na kujadiliwa ipasavyo na Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

2.1 Maelezo ya jumla kuhusu uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, masharti ya Kanuni za Bunge² na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali katika aya 1.3. na 1.4, uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma umechambuliwa kwa ufasaha na kwa kina katika aya zinazoanzia na namba 2.2.

2.2 Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo: -

2.2.1 Tathmini ya ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura ya 399 na ilianza utendaji wake wa kazi mnamo tarehe 01 Julai 1999. TRA imekabidhiwa jukumu la msingi la Kisheria la kukusanya kodi mbalimbali hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano (2015 – 2020) TRA imeongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya Kisheria ambapo kati ya mwaka 2016 hadi 2019, TRA imefanikiwa kukusanya mapato kwa wastani wa asilimia 88.1 ukilinganisha na malengo ambayo wamekuwa wakipewa.

² Rejea masharti ya Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016

Hii ni hatua kubwa inayoashiria ufanisi wa kiutendaji na ongezeko la wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio hayo, uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2019 umebaini changamoto katika maeneo makuu mawili ambayo yanachangia kutokusanywa mapato stahiki ya Serikali. Eneo la kwanza ni dosari za kiusimamizi katika Idara ya ushuru na forodha (*Customs and excise department*) na eneo la pili ni uwepo wa mashauri mengi ya kodi (*Tax objections and appeals*) ambayo hayaitimishwi kwa wakati pamoja na changamoto katika ukusanyaji wa madeni ya kodi (*Tax arrears*).

Mheshimiwa Spika, Katika Idara ya ushuru na forodha, Kamati imebaini hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 kiasi cha fedha cha jumla ya **shilingi 712,452,893,804.42** kilikuwa hakijakusanywa kutokana na sababu mbalimbali. Mchanganuo wa fedha hizo na sababu za kutokusanywa kwa fedha husika umefafanuliwa katika jedwali Namba 2.1 hapa chini: -

Jedwali Na. 2.1 Mapato ambayo hayakukusanywa na TRA kutokana na dosari mbalimbali katika Idara ya ushuru na forodha hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020

Na	Sababu ya kutokusanywa	Jumla (TZS)
1.	Bidhaa zinazosafirishwa Nje ya Nchi (<i>On transit goods</i>) lakini hazikuwa na uthibitisho wa kutoka hapa Nchini	127,883,079,456.06
2.	Mafuta ya liyoagizwa kutumika hapa Nchini bila kuwa na uthibitisho wa malipo ya kodi na riba	265,286,247,887.00
3.	Bidhaa zilizoagizwa na kupatikanakuwa na dosari katika mchakato wa forodha	88,554,112,085.70
4.	Bidhaa zilizoagizwa kwa malengo ya kuuzwa Nje ya Nchi lakini zikabaki hapa Nchini	228,474,766,766.66
5.	Bidhaa zilizoagizwa kwa matumizi ya muda hapa Nchini lakini zimekosa uthibitisho wa kusaafirishwa Nje ya Nchi	2,254,687,609.00
JUMLA		712,452,893,804.42

Chanzo: Taarifa ya CAG ya ukaguzi wa TRA kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019

Mheshimiwa Spika, Kama jedwali namba 2.1 linavyofafanua hapo juu, kiasi kikubwa cha fedha za kodi kilikuwa kimehojiwa na CAG na kilikuwa hakijakusanywa hadi mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2019. Changamoto kubwa katika Idara ya ushuru na forodha ni suala la ufuatiliaji wa karibu wa taratibu za forodha pamoja na kutofanyika usuluhishi (*Tax reconciliation*) wa makusanyo ya kodi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Eneo la pili ambalo Kamati kwa kipindi chote cha miaka mitano imekuwa ikilitolea msisitizo ni uwepo wa mashauri mengi ya kodi (*Tax objections and appeals*) ya muda mrefu ambayo hayaitimishwi kwa wakati na dosari katika makusanyo ya madeni ya kodi (*Tax arrears*) hali ambayo inaipotezea Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 jumla ya mashauri ya kodi yenye thamani ya **shilingi 84,615,063,093** yalikuwa hayajahitimishwa. Hali hii kwa kiasi kikubwa inachangiwa na vyombo vinavyohusika na utoaji wa maamuzi ya kodi, Bodi ya Rufaa ya Kodi (³TRAB) na Baraza la Rufaa za Kodi (⁴TRAT) kutotekelezwa majukumu yake ya Kisheria kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mathalani, kwa mwaka huu tunaoutolea taarifa, Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) haikuwa na ⁵Makamu Mwenyekiti ambaye anawakilisha Tanzania Zanzibar. Aidha, kwa upande wa Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT), CAG alibaini kuwa kulikuwa na nafasi ⁶kumi za wajumbe ambao walikuwa hawajateuliwa. Kwa msingi huo, kwa nyakati tofauti kulikuwa na uwezekano wa Baraza kutofanya vikao vyake kwa kukosa akidi inayotakiwa kama Kifungu cha 14(1) cha Kanuni za TRAT za mwaka 2018 kinavyoelekeza.

³ Tax Revenue Appeal Board

⁴ Tax Revenue Tribunal Board

⁵ Refer Section 24 (a) of the Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, 2016

⁶ Refer Section 26 (b) of the Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, 2016

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa changamoto ya ukusanyaji wa madeni ya kodi za siku za nyuma (*Tax arrears*), hadi kufikia tarehe 20 Aprili, 2020 jumla ya deni la kodi la kiasi cha ⁷**shilingi 303,091,352,906** lilikuwa bado halijakusanywa na TRA.


Mheshimiwa Spika, Maeneo yaliyofafanuliwa hapo juu ni ya muhimu sana kushughulikiwa kwa wakati mwafaka. Kwa kufanya hivyo ufanisi wa TRA uliojitokeza katika miaka mitano iliyopita utaongezeka zaidi.

2.2.2 Madeni ambayo TANESCO inadai kwa taasisi za Serikali na wateja binafsi bilioni 454.4

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilikuwa linadai jumla ya shilingi **bilioni 454.4** kutoka kwa wateja mbalimbali. Mchanganuo wa deni hilo unafafanua kwamba, taasisi mbalimbali za Serikali zinadaiwa jumla ya shilingi **bilioni 205.8**, wateja binafsi **shilingi bilioni 199.3** na madeni mengineyo jumla yake ni **shilingi bilioni 49**.

Mheshimiwa Spika, Mgawanyo wa deni hilo umefafanuliwa katika chati namba 2.1 hapa chini: -

Chati Na. 2.1: Mchanganuo wa deni ambalo TANESCO inadai kwa wateja mbalimbali Mchanganuo wa madeni ambayo TANESCO inadai



Chanzo: Taarifa ya ukaguzi wa hesabu za TANESCO kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2019

⁷ Rejea Uk. iv wa Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa Serikali Kuu kwa Mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Athari ya uwepo wa deni lililobainishwa katika chati Na. 2.1 hapo juu, ni kupungua kwa hali ya ukwasi (*Liquidity*) wa TANESCO na hivyo kuathiri hali ya kiutendaji ya Shirika hilo muhimu kwa maendeleo ya Taifa. Pamoja na jitihada kubwa za ongezeko la mapato ya TANESCO kwa siku za hivi karibuni, deni ambalo halijakusanywa linaathiri uwezo wa TANESCO kugharamia shughuli mbalimbali kwa pale inapotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kutokusanywa kwa deni hilo pia kuna athari katika taarifa za hesabu za TANESCO (*Financial statements*) kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za hesabu (*International financial reporting standards, IFRS*). Kwa mujibu wa ⁸Kifungu cha 9 cha IFRS, TANESCO inatakiwa kuainisha hasara ya wastani wa asilimia 5 hadi 10 kwa madeni ambayo yamedumu kwa muda mrefu bila kukusanywa (*Expected credit loss*).

Mheshimiwa Spika, Ni kwa msingi huo, jitihada za TANESCO kusafisha taarifa za hesabu zake ikiwa ni pamoja kufuta hasara ya muda mrefu hazitafanikiwa kwani nakisi (*Deficit*) itaendelea kuonekana sababu ya deni ambalo TANESCO inadai na halijakusanywa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa madeni haya kukusanywa kwa wakati ili kuipa TANESCO uwezo wa kujiendesha ili kusaidia dhima ya Tanzania kuwa Nchi ya viwanda.

2.2.3 Usimamizi wa mikataba na hali ya ufanisi katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)


Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha kati ya mwaka 2015 hadi 2020, Kamati imekuwa ikitoa mapendekezo kadhaa yenye lengo la kuboresha shughuli za Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA). Mapendekezo hayo yamesaidia kuongeza

⁸IFRS 9 requires an entity to recognize a financial asset or a financial liability in its statement of financial position when it becomes party to the contractual provisions of the instrument

ufanisi wa TPA ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa shehena ya mizigo inayohudumiwa na TPA kwa wastani wa asilimia 2.1 kwa mwaka pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2018-2019 shehena iliyohudumiwa na Bandari za TPA ilikuwa tani za uzito **17,166,079** ikilinganishwa na tani za uzito **16,197,818** zilizohudumiwa mwaka 2017/18 hili ni ongezeko la tani za uzito **968,261** sawa na asilimia **6.0**. Mwenendo wa ongezeko la shehena umefafanuliwa katika chati Na. 2.2 hapa chini:-

Chati Na. 2.2: Mwenendo wa shehena zilizohudumiwa na TPA kati ya mwaka 2015 - 2019



Chanzo: Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TPA kwa mwaka 2019

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio hayo na ongezeko la shehena ya mizigo iliyohudumiwa kama chati Na. 2.2 ilivyofafanua, Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa changamoto kadhaa katika TPA ambazo zinapunguza ufanisi wa Mamlaka. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

a) Changamoto za kimfumo ambazo bado hazijapata ufumbuzi wa kudumu. Kwa mwaka huu CAG amebainisha

mapungufu kadhaa katika mfumo wa makusanyo ya fedha ya bandari (*TPA billing system*). Mapungufu hayo yamesababisha dosari kadhaa ikiwamo uwepo wa **shilingi bilioni 2** ambazo ni tofauti ya fedha ambayo haikuwa imefanyiwa usuluhishi na hati za madai za **shilingi bilioni 1.8** ambazo hazikupatikana wakati wa ukaguzi;

b) Dosari katika usimamizi wa mikataba, ambapo katika mikataba 7 iliyokaguliwa, CAG alibaini kutokuwepo taarifa za maendeleo ya miradi (*Project progress reports*). Suala hili ni kinyume na matakwa ya Kanuni ya 243 (1) ya ⁹Kanuni za Manunuzi ya Umma (PPR) za mwaka 2013 kama zilivyorekebisha mwaka 2016; na

c) Ongezeko la deni ambalo TPA inadai kwa wateja kwa mwaka 2019 ambapo CAG amefafanua deni hilo kwa Bandari ya Dar es Salaam lilikuwa **shilingi bilioni 25**. Hii ni kinyume na **Kifungu 3.3.3** cha kanuni za fedha za TPA ambacho kinataka huduma zote za Bandari zilipiwe kwa fedha taslim.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na changamoto tulizobainisha hapo juu, CAG ameifahamisha Kamati kuwa ameanza zoezi la ukaguzi maalum (*Special audit*) katika eneo la ununuzi (*Purchasing*), usimikaji (*Installing*) na utendaji (*Performance*) wa mifumo mbalimbali ya shughuli za TPA. Ukaguzi huu ni muhimu ukakamilika kwa wakati ili uweze kusaidia udhibiti wa matumizi na mapato ya Serikali.

2.2.4 Matumizi yasiyo na manufaa (*Nugatory expenditure*) ya shilingi 1,083,301,547 katika Wakala wa Umeme Vijijini (REA)

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG umebaini kuwa REA waliingia mkataba na Kampuni ya

⁹Reg. 243. -(1) of PPR 2013 (as amended in 2016) In the case of contracts for non-consultant services or works, a procuring entity shall monitor the service provider or contractor's performance against the statement of requirements or schedule of works stated in the contract, by means of daily, weekly or monthly reports from the procuring entity's supervisor responsible for the services or works

SMEC INTERNATIONAL PTY LTD kwa ajili ya shughuli za ushauri wa kitaalam. Shughuli hizo zilihusu uandaaji wa nyaraka za zabuni (*Bid documents*) kwa ajili ya ushauri na usanifu wa kina wa ujenzi wa njia ya mkondo wa kati wa umeme "*Medium voltage*" kwaajili ya vijiji **7,893** hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya ushauri ambayo ingetolewa na Kampuni hiyo ya ushauri ingetumiwa na wakandarasi 29 ambao wangehusika na kuwaunganishia umeme wanavijiji katika vijiji **7,893**. Gharama ambazo Kampuni hiyo ililipwa ni jumla ya **shilingi 1,083,301,547**.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, kabla Kampuni husika haijakamilisha taarifa ya ushauri, REA na TANESCO waliteua wakandarasi 29 kuanza kutekeleza miradi husika. Kwa msingi huo Kampuni ya **SMEC INTERNATIONAL PTY LIMITED** ililipwa fedha kwa kuandaa taarifa ambayo REA na TANESCO hawakuitumia katika utoaji wa zabuni kwa wakandarasi husika.

Mheshimiwa Spika, Ni kwa msingi huo, CAG ametoa maoni kuwa, malipo hayo ya **shilingi 1,083,301,547** ni malipo yasiyokuwa na manufaa kwa Wakala (*Nugatory expenditure*). Aidha, CAG amependekeza hatua za uchunguzi kuhusu malipo hayo ambayo yana viashiria vya matumizi yasiyofaa ya fedha za umma.

2.2.5 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya ukaguzi ya CAG kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) umebaini mapungufu katika maeneo makubwa mawili. Maeneo hayo ni dosari katika utunzaji wa malighafi za kuzalisha vitambulisho vya Taifa zenye thamani ya **shilingi bilioni 42** na eneo la pili ni kutokuwepo kwa mikataba kati ya NIDA na watumiaji wa taarifa za NIDA hivyo kuikoshesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, Katika dosari ya utunzaji wa malighafi ya vifaa vya kutengeneza vitambulisho vya Taifa, masuala yafuatayo yalibainika: -

a) Kutokuwepo kwa taarifa sahihi za mahitaji ili kubaini mahitaji halisi ya vifaa vya kutengeneza vitambulisho (*Poor management of stock levels*);

b) Uwepo wa malighafi ya ziada ikilinganishwa na mahitaji halisi ya utengenezaji wa vitambulisho vya Taifa ambayo haiwezi kutumika hivi karibuni. Kiasi kilichokuwepo tarehe 30 Juni, 2019 ni vipande **5,411,500** vyenye thamani ya **shilingi 42,624,536,046.00**, kiasi hiki kinaweza kutumika kwa siku **677** sawa na mwaka **mmoja** na miezi **nane** kwa uzalishaji wa kadi **8,000** kwa siku;

c) Kukosekana eneo linalofaa kuhifadhia vifaa badala yake vinahifadhiwa chini ya sakafu; na

d) Kadi zilizoharibika zinahifadhiwa pamoja na ambazo hazijatumika hali inayochangia kuwepo kwa upotevu na ugumu wa kutambua kadi zilizotumika na ambazo bado hazijatumika.

Mheshimiwa Spika, Eneo la pili ambalo Kamati ilibaini katika NIDA ni kutokuwepo kwa mikataba kati ya NIDA na taasisi zinazotumia taarifa za NIDA. Kifungu 4.9.2 cha Mpango Mkakati (*Strategic plan*) wa miaka mitano wa NIDA (2019/2020 – 2023/2024) unaitaka NIDA kufanya tathmini ili kuongeza mapato kupitia kuingia hati za makubaliano (MOU) kati yake na taasisi zinazotumia taarifa zake.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi sasa, NIDA wamekuwa wakichangia matumizi ya taarifa zake na taasisi binafsi 41 na 26 za umma kwa matumizi mbalimbali bila ya kuwa na mikataba au hati za makubaliano (MOU).

Mheshimiwa Spika, Kutokuwepo mikataba au makubaliano rasmi na watumiaji kutoka taasisi hizo kunaikosha Serikali tozo ambayo ingepatikana kutoka kwa watumiaji. Aidha, Serikali inakosa nafasi ya kuchukua hatua kwa watumiaji kitokea wamekiuka masharti ya matumizi waliyoomba.

2.2.6 Matokeo ya ukaguzi maalum kuhusu mali na madeni ya Kampuni ya Pride

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 04 Julai, 2019, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango alimuandikia barua CAG kuomba kufanyika ukaguzi maalum wa mali na madeni ya Kampuni ya Pride. Aidha, katika kipindi hicho Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) pia ilimuomba CAG kufanya ukaguzi maalum katika Kampuni ya Pride kwa hadidu za rejea walizopendekeza.

Mheshimiwa Spika, Timu ya wakaguzi ilizingatia taarifa ya ukaguzi wa Kampuni ya Pride kwa tarehe 31 Disemba, 2016 uliokuwa umefanywa na Kampuni ya Ernest & Young pamoja na malipo yaliyokuwa yamefanyika kati ya tarehe 01 Januari, 2017 hadi tarehe 31 Oktoba, 2019. Aidha, wakaguzi waliangalia historia ya uanzishwaji wa Kampuni ya Pride tangu mwaka 1988, taarifa za usajili wake, umiliki na hali halisi ya Kampuni kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kuzingatia matokeo ya ukaguzi huo maalum, Kamati imeona ni suala la muhimu Bunge lako Tukufu likajulishwa kwa kina namna Kampuni ya Pride ilivyotumia vibaya fedha za umma. Kwa muhtasari CAG alibaini yafuatayo katika Kampuni ya Pride: -

a) Katika Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya tarehe 31 Disemba 2016, Kampuni ya Pride ilikuwa na akiba katika Benki kiasi cha **shilingi 428,306,662**. Hata hivyo, ukaguzi maalum kupitia taarifa za Benki (*Bank statements*) zinazoishia tarehe 31 Oktoba 2019 ulibaini kwamba hakuna salio lolote lililobakia katika akaunti za Kampuni ya Pride;

b) Kampuni ya Pride iliwekeza hisa katika Bank M (Tanzania) Limited kiasi cha hisa **4,762,237** kwa **shilingi 400** kwa kila hisa ambapo thamani yake ni jumla ya **shilingi 1,904,894,800**. Hata hivyo, Kampuni ya Pride ilitumia hisa hizo kama dhamana ili kupata mikopo kutoka Bank M. Thamani ya hisa hizo iliongezeka kutoka **shilingi 1,904,894,800** mwaka 2015 hadi **shilingi 2,310,610,800** mwaka 2016, ongezeko hili lilitokana na

kupewa hisa za ziada zenye thamani ya kiasi cha **shilingi 405,000,000**. Hii ni kwa mujibu wa taarifa za Mkaguzi wa hesabu (Ernst & Young) za tarehe 31 Disemba 2016. Hata hivyo, ukaguzi maalum umebaini Benki ya Azania ambayo inasimamia Bank M kwa sasa haina taarifa zozote kuhusu uwepo wa hisa hizo;

c) Taarifa ya Mkaguzi wa hesabu (*Ernst & Young*) ya tarehe 31 Disemba 2016 inaonyesha uwepo wa dhamana zilizowekwa na Kampuni ya Pride katika Benki ya CRDB kiasi cha **shilingi 29,525,699,342**, Bank M/Azania Bank Ltd kiasi (cha **shilingi 15,284,381,700** na riba ya dhamana hizi kiasi cha **shilingi 3,400,599,793**. Hata hivyo, ukaguzi maalum umebaini kuwa dhamana hizo zilitumika kupunguza mikopo iliyokuwa imechukuliwa na Pride katika mabanki husika;

d) Ukaguzi maalum umebaini jumla ya kiasi cha **shilingi 11,148,285,088** ni madeni yaliyochukuliwa na watumishi wapatao **209** bila kurejeshwa hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2019. Katika madeni hayo kuna watumishi wapatao **168** walioacha/kuachishwa kazi kabla ya kumaliza madeni yao kiasi cha **shilingi 745,592,061**, kuna watumishi **8** waliopo Kampuni ya Pride wanaodaiwa hadi sasa kiasi cha **shilingi 15,761,415**, kuna kiasi cha **shilingi 2,602,189,409.36** hakikuwa na maelezo ya mkopaji wala matumizi ya fedha hizo na pia kuna madeni ya watumishi **33** yaliyokuwa hayajakatwa kwenye mishahara ambayo ni kiasi cha **shilingi 10,386,931,612**;

e) Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba 2019, Kampuni ya Pride inadaiwa jumla ya kiasi **cha shilingi 130,149,148,000**. Fedha hizi ni mikopo kwa Taasisi za fedha za Ndani na Nje ya Nchi, amana za wateja, malipo ya bima na watoa huduma wengine;

f) Ukaguzi maalum ulibaini ubadhirifu wa fedha uliofanywa na baadhi ya watumishi wa Kampuni ya Pride kiasi cha **shilingi 10,465,476,612**; na

g) Ubadhirifu wa fedha za malipo ya watoa huduma mbalimbali kwa huduma ambazo hazikufanyika Kampuni ya Pride kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka 2017 **shilingi 585,935,080**.

Mheshimiwa Spika, Kwa muhtasari hayo ndiyo maeneo muhimu ambayo CAG amebainisha katika ukaguzi wake maalum wa Kampuni ya Pride. Kiwango cha fedha kilichopotea katika Kampuni hiyo ni kikubwa ambacho kingesaidia maendeleo ya Taifa letu. Kamati inasisitiza na kuishauri Serikali kutekeleza mapendekezo yote ya ukaguzi kama yalivyotolewa na CAG.

2.2.7 Matumizi ya shilingi 1,511,995,098 katika Wizara ya Maliasili na Utalii bila ya kuwepo kwenye mpango wa bajeti

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 4(1) ya Kanuni za fedha za umma za mwaka 2001 kama zilivyorekebishwa mwaka 2004 zinalipa Bunge Mamlaka ya kupitisha na kuidhinisha matumizi yeyote ya fedha za Serikali. Nukuu ya Kanuni hiyo ni kama ifuatavyo: -

“ For purposes of having the control of public money the National Assembly shall be vested with exclusive right to authorize public expenditure, through the approval of annual estimates expenditure and the enactment of Appropriations Acts”

Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa, Wizara ya Maliasili na Utalii ilikusanya fedha kutoka taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hiyo kiasi cha **shilingi 1,511,995,098** kwaajili ya shughuli za Tamasha la Utalii “ *Utalii Festival*”. Tamasha hilo lilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Manyara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na nia njema ya Wizara katika kukuza utalii kupitia tamasha husika, CAG amefafanua kuwa fedha hizo zilitumika bila ya kuwa kwenye mpango wa bajeti ya Wizara na pia zilitumika kabla ya kupata vibali husika. Aidha, hoja ya ukaguzi inabainisha kuwa fedha hizo zilitumika

bila idhini ya Bunge kama Kanuni za fedha za umma zinavyoelekeza. Mchanganuo wa malipo ya fedha hizo umechambuliwa katika jedwali Na. 2.2 hapa chini: -

Jedwali Na. 2.2: Mchanganuo wa matumizi ya shilingi 1,511,995,098 katika fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Na.	Maelezo ya matumizi	Kiasi (TZS)
1.	Malipo kwenda kwa taasisi nyinginezo	479,758,000
2.	Malipo wa kwa wazabuni	643,462,814
3.	Malipo kwa vikundi vya sanaa na wasanii	52,157,500
4.	Posho ya kujikimu kwa watumishi wa Wizara na kikosi kazi	135,153,000
JUMLA		1,511,995,098

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi ya fungu 69 Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2019

Mheshimiwa Spika, Matumizi tajwa hapo juu, kwa kiasi kikubwa yanaathiri mfumo wa malipo wa Serikali (IFMS – Epicor). Aidha, kwa utaratibu uliotumika kukusanya fedha hizo bila ya kuwa kwenye mpango wa bajeti kunaweza kusababisha matumizi yasiyofaa ya fedha za umma na kuathiri utekelezaji wa shughuli nyinginezo zilizokuwa zimekasimiwa kwa mwaka husika.

2.2.8 Hali ya kifedha ya Benki zinazomilikiwa na Serikali

Mheshimiwa Spika, Benki zinazomilikiwa na Serikali ni vyombo muhimu vilivyoanzishwa kwaajili ya kuchochea maendeleo katika nyanja mbalimbali. Benki hizi pamoja na kufanya biashara kwa kuhudumia wananchi, zinatumiwa pia na Serikali kimkakati katika kugharamia miradi muhimu ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa Benki 4 za biashara ambazo zinamilikiwa na Serikali; Benki hizo ni Benki ya Benki ya Uwekezaji (Maendeleo), Benki ya Benki ya Uwekezaji (Biashara), Benki ya Posta Tanzania (TPB) na Benki ya Kilimo (TADB). Benki hizi zinamilikiwa na Serikali kwa asilimia

100. Benki hizo za Serikali zimekuwa zikitekeleza majukumu mahsusi kama ifuatavyo: -

- a) Kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na maendeleo;
- b) Kutoa huduma za kibenki kwa ajili ya shughuli maalum za uwekezaji;
- c) Kutoa ushauri na huduma za masoko ya mitaji na uwekezaji (*brokerage and investment services*);
- d) Kusimamia fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli maalum za uwekezaji; na
- e) Kutoa misaada na ushauri wa kitaalam ili kuendeleza shughuli zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika mwenendo wa Benki za Serikali katika mwaka 2019 ulibaini kuwa Benki ya Uwekezaji (Biashara) na Benki ya Uwekezaji (Maendeleo) zina changamoto kubwa ya mtaji. Hali hiyo inatatiza utendaji wenye ufanisi na malengo ya kuanzishwa Benki hizo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ya mtaji, Benki ya Uwekezaji (Maendeleo) na Benki ya Uwekezaji (Biashara) zinaweza kupewa adhabu na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na hata kufungwa leseni ya biashara kwa kukiuka ¹⁰miongozo muhimu inayosimamia shughuli za Benki hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Benki ya Uwekezaji (Maendeleo) mtaji wake upo chini ya kiwango cha mwongozo wa BOT katika masuala ya kugharamia shughuli za uwekezaji. Mwongozo huo ukisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 19(2) ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha, unaitaka Benki wakati wowote kudumisha kiasi cha chini cha

¹⁰ Kanuni ya 9(a) na (b) za Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Utoshelevu wa Mtaji) za Mwaka 2014 na Mwongozo Na. FA.43/433/01/Vol. III wa Benki Kuu ya Tanzania wa tarehe 5 Agosti 2015

mtaji wa msingi na mtaji wa jumla usiopungua asilimia 12.5 na 14.5 mtawalia, wa jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi na mali zilizo katika hali hatarishi zilizo nje ya urari wa kimahesabu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG ulibaini kuwa, kwa Benki ya Uwekezaji (Maendeleo) uwiano wa kiasi cha chini cha mtaji wa msingi na mtaji wa jumla upo katika **(13% na 15%)**. Aidha, kwa Benki ya Uwekezaji (Biashara) uwiano huo upo kwa **(12.5% na 14.5%)**.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mapungufu ya mtaji, Benki hizo mbili zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya mikopo chechefu (¹¹NPL), gharama kubwa za riba katika kupata mikopo, changamoto katika utekelezaji uandaaji taarifa za hesabu kwa viwango vya kimataifa (Hususan ¹²IFRS 9) na ushindani wa soko.

2.2.9 Kutofanyika tathmini ya uwezo wa mfuko wa PSSF (Actuarial valuation)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa pensheni kwa watumishi wa umma (PSSF) ulianzishwa rasmi mnamo tarehe 01 Agosti, 2018. Mfuko wa PSSF ulitokana na uamuzi wa Serikali kuunganisha mifuko ya pensheni 4 iliyokuwepo hapo awali. Mifuko hiyo ni PSPF, PPF, GEPF na LAPF.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kuunganishwa kwa mifuko hiyo na kuwa PSSF, CAG alitoa mapendekezo kuwa ni muhimu kukafanyika tathmini ya kitaalamu ya kutambua uwezo wa mfuko wa PSSF kuweza kutimiza majukumu yake ya kulipa pensheni kwa siku zijazo. Zoezi hili hufahamika kitaalamu kama "¹³Actuarial valuation".

¹¹ Non - performing loans

¹² IFRS 9 requires an entity to recognize a financial asset or a financial liability in its statement of financial position when it becomes party to the contractual provisions of the instrument

¹³ An actuarial valuation is an analysis performed by an actuary that compares the fair value of assets and liabilities of a pension plan

Mheshimiwa Spika, Hadi ukaguzi wa mwaka 2019 unakamilika, zoezi hilo la tathmini lilikuwa halijakamilika. Athari ya kutofanyika kwa zoezi hilo muhimu ni kwamba, mfuko unakosa tathmini ya kina iwapo una uwezo wa kulipa mafao siku zijazo kwa kutumia rasilimali ilizonazo sasa. Aidha, zoezi hilo hutumika kama nyenzo muhimu ya kufanya maamuzi kuhusu masuala kama uwekezaji na maboresho ya mafao mbalimbali.

2.2.10 Kutosainiwa kwa hesabu za Shirika la Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) baada ya kutolewa hati isiyoridhisha (Qualified audit opinion)

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Simu Tanzania (TTCL) ulikamilika mnamo mwezi Disemba, 2019. Katika ukaguzi huo, CAG alitoa hati isiyoridhisha (*Qualified audit opinion*) kwa hesabu za TTCL. Hata hivyo, kinyume na masharti ya Kifungu cha 13 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008, Bodi ya TTCL haikupokea na kuridhia (*Adopt*) taarifa husika ya ukaguzi iliyokuwa na hati iliyopendekezwa, ili baadaye isainiwe na CAG. Aidha, Bodi iliitaka Menejimenti kurudi kufanyia kazi hoja za ukaguzi. Kwa hatua hiyo, hesabu za TTCL hazikurudi kwa CAG kwa muda mwafaka hadi wakati anatoa taarifa yake ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, Katika kujadili hoja hii mnamo tarehe 18 Mei, 2020 Dodoma, Kamati ilikuwa na maoni kuwa, Bodi ya TTCL kutopokea na kuridhia taarifa ya ukaguzi kwa wakati kwa sababu ya hoja zilizomo na hati ya ukaguzi iliyokuwa imependekezwa ni hali ya kuingilia uhuru wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT). Kifungu cha 13 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma (2008) kimefafanua suala hilo kwa ufasaha. Nukuu ya Kifungu hicho cha Sheria ni kama ifuatavyo: -

“The independence and status of the Office of the Controller and Auditor General shall be as provided for under Article 143 of the Constitution.” Mwisho wa nukuu.

Mheshimiwa Spika, Masuala muhimu yaliyosababisha CAG kutoa hati isiyoridhisha kwa TTCL ni haya yafuatayo: -

a) Utofauti wa kiasi kikubwa cha fedha katika taarifa za makusanyo katika mifumo ya TTCL. Kampuni ina mifumo miwili ya ukusanyaji mapato (¹⁴CVBS na SUN). CAG alibaini uwepo wa tofauti ya **shilingi bilioni 1.75** katika mifumo hiyo;

b) Uwepo wa kiasi cha **shilingi 11,101,916,226** ambacho kilionekana kuwa deni ambalo TTCL inadaiwa na wateja wake. Jambo hili sio la kawaida kwa TTCL kudaiwa kiasi hicho kikubwa cha fedha na wateja. Aidha, CAG hakupata nyaraka za kuthibitisha usahihi wa deni hilo;

c) Kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho wa deni la **shilingi bilioni 91.43** ambalo TTCL inadai kwa wateja mbalimbali; na


d) Kutofanyika usuluhishi wa madeni mbalimbali, utunzaji wenye dosari wa vitabu vya hesabu na uandaaji wa taarifa za hesabu zenye mapungufu.

Mheshimiwa Spika, Changamoto za utunzaji wa hesabu katika TTCL kama ilivyofafanuliwa hapo juu ni kihatarishi cha juu (*High risk area*) katika kuongeza ufanisi wa Kampuni hiyo. Aidha, hatua ya Bodi ya TTCL kutopokea na kuridhia taarifa ya hesabu zilizokaguliwa ili zikasainiwe na CAG kwa wakati kama sheria inavyoelekeza, ina athari kubwa katika suala la uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, TTCL inahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa ili kuiongezea ufanisi. Hii inadhihirishwa na nafasi ndogo ya TTCL katika soko la huduma za simu za mkononi (*Market share*) hapa Nchini kama ilivyofafanuliwa katika: Na. 2.3.

¹⁴ Convergent billing system

Chati Na. 2.3: Nafasi ya TTCL katika soko la huduma za simu za mkononi hapa Nchini



Chanzo: Taarifa ya CAG kwa hesabu za TTCL kwa mwaka unaoshia 30 Juni, 2019

Mheshimiwa Spika, Taswira inayoonekana katika chati Na. 2.3 ikibainisha nafasi ya TTCL katika soko la simu za mkononi hapa Nchini, ndiyo msingi wa Kamati kuendelea kusisitiza umuhimu wa kufanyika mabadiliko makubwa ya kiuendeshaaji katika TTCL. Mabadiliko hayo yatasaidia kuiondoa Kampuni katika nafasi ya wastani wa asilimia 1 katika soko la huduma za simu za mkononi hapa Nchini kwa kuwa ina kila nafasi ya kuongeza soko na ufanisi.

2.2.11 Kutolewa Hati mbaya ya ukaguzi (*Adverse opinion*) kwa Kampuni ya STAMIGOLD

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa ukaguzi 2018/2019, Kampuni ya STAMIGOLD ilipata hati mbaya ya ukaguzi (*Adverse opinion*). Hati mbaya ya ukaguzi hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hii inaathiri taarifa za fedha kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya STAMIGOLD ilipata hati mbaya ya ukaguzi (*Adverse opinion*) kutokana na masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Kutokuwepo kwa uthibitisho wa deni la jumla ya **shilingi bilioni 52.5** ambalo Kampuni ya STAMIGOLD inadaiwa kama lilivyobainishwa katika **“note 27”** ya taarifa za hesabu. CAG hakupata nyaraka yeyote ya kuthibitisha usahihi wa deni hilo; na

b) Kutokuwepo kwa uthibitisho wa deni la jumla ya **shilingi bilioni 52.5** ambalo Kampuni ya STAMIGOLD inadai kwa kampuni mbalimbali kama lilivyobainishwa katika **“note 12”** ya taarifa za hesabu. CAG hakupata nyaraka yeyote ya kuthibitisha usahihi na mkakati wa ukusanyaji wa deni hilo.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na CAG kutoa hati mbaya alitoa pia eneo la msisitizo katika taarifa ya hesabu za Kampuni ya STAMIGOLD. Eneo la msisitizo linahusu uendelevu wa baadaye wa shughuli za Kampuni (*Going concern*).

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya hesabu za Kampuni ya STAMIGOLD umebaini kuwa, Kampuni ilipata hasara ya shilingi **bilioni 2.80** kwa mwaka 2019 (**shilingi bilioni 16.4**, mwaka 2018). Pamoja na kupungua kwa hasara, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa madeni ya Kampuni yanazidi rasilimali za Kampuni kwa **shilingi bilioni 39.36**. Tafsiri ya uwiano huo (mali na madeni), ni dhahiri Kampuni ya STAMIGOLD haina uwezo wa kugharamia shughuli zake za muda mfupi kwa rasilimali walizo nazo kwa sasa.

2.2.12 Matumizi ya Bodi za Mazao kuzidi mapato hivyo kutofikiwa malengo

Mheshimiwa Spika, Tangu uhuru, Serikali imekuwa ikisaidia sekta ya kilimo ikihusisha pia kuanzisha taasisi mbalimbali za kilimo ambazo zimepewa mamlaka ya kutekeleza majukumu ambayo yanaweza kupunguza changamoto zilizotajwa katika MKUKUTA awamu ya pili. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa masoko kwa Wakulima, changamoto za

huduma za ugani na kutofikiwa kwa mnyororo wa uzalishaji wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hizo ni pamoja na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Bodi ya Kahawa (TCB), na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (Nafaka) (CBP).

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingine ni pamoja na mifuko ya maendeleo ya mazao kama Mfuko wa Kahawa, Mfuko wa Korosho, na Mfuko wa Pamba ambayo hivi karibuni ilivunjwa na majukumu yake kuhamishiwa kwenye bodi za mazao husika.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuundwa kwa taasisi hizi, bado kuna changamoto zinazozikumba taasisi na bodi hizi. Changamoto kubwa ambayo CAG ameibainisha ni matumizi makubwa ya bodi hizo kuliko uwezo wa mapato. Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018 - 2019 ulibaini kati ya bodi za mazao 9; bodi 5 sawa na 56% zilikuwa na nakisi kwenye mwaka huo hivyo kuathiri utendaji kazi wa bodi hizo. Jedwali Na. 2.3 linatoa ufafanuzi wa mapato, matumizi na bakaa/nakisi kwa bodi 9 za mazao hapa Nchini: -

Jedwali Na. 2.3 Mchanganuo wa mapato, matumizi na bakaa/ nakisi katika bodi 9 za mazao hapa Nchini

Na.	Jina la Bodi	Mapato	Matumizi	Bakaa/ nakisi
1.	Bodi ya Sukari Tanzania	6,835,693,000	5,635,191,000	1,200,502,000
2.	Bodi ya Chai Tanzania	649,428,253	818,667,905	(169,239,652)
3.	Bodi ya Korosho Tanzania	4,729,543,000	6,847,443,000	(2,117,900,000)
4.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	2,343,317,584	2,490,484,811	(147,167,227)
5.	Bodi ya Mkonge Tanzania	367,535,626	489,896,998	(122,361,372)
6.	Bodi ya Kahawa Tanzania	5,914,990,000	5,039,745,000	875,245,000
7.	Bodi ya Mazao Mchanganyiko	647,850,779,073	25,981,094,020	621,869,685,053
8.	Bodi ya Pareto Tanzania	248,826,200	264,740,770	(15,914,570)
9.	Bodi ya Pamba Tanzania	4,920,672,000	4,881,363,000	39,309,000

Chanzo: Taarifa ya ukaguzi ya CAG kwa Bodi za Mazao hadi kwa mwaka wa fedha unaoshia Juni 30, 2019

Mheshimiwa Spika, Kama jedwali Na. 2.3 hapo juu linavyofafanua, kati ya bodi 9 za mazao zilizokaguliwa, bodi 5 zimekuwa na nakisi (*Deficit*) katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika hali hiyo, ni dhahiri kwamba ufanisi wa kiutendaji katika bodi unaweza kushuka.

2.2.13 Uwekezaji katika Kampuni ya Mkulazi

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mkulazi inamilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa asilimia 96 na Jeshi la Magereza kwa asilimia 4. Kutokana na taarifa ya upembuzi yakinifu ya mwezi Januari mwaka 2019, CAG alibaini kuwa, Kampuni ilipaswa ianze uzalishaji wa sukari katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, hadi CAG anakamilisha ukaguzi mwezi Desemba 2019, Kampuni ilikuwa haijaanza uzalishaji. Hali hii imepelekea Kampuni kupata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2019, Kampuni ilikuwa imepata hasara ya jumla ya **shilingi bilioni 8.87** sawa na **asilimia 30** ya kiasi kilichowekezwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kuchelewa kufunga mitambo ya uzalishaji sukari. Kutokana na kuchelewa huko, Kampuni ya Mkulazi ililazimika kuuza miwa kwa bei ya chini ukilinganisha na bei ya uzalishaji.

2.2.14 Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Kwa taarifa ya ukaguzi ya mwaka 2019, Kamati ilichambua taarifa ya hesabu za BOT na kubaini eneo moja ambalo BOT inatakiwa kulifanyia kazi kwa msisitizo.

Mheshimiwa Spika, Eneo hilo linahusu BOT kuchukua muda mrefu kuhesabu fedha zinazotoka kwenye Benki za Biashara. Kwa mwaka huu hadi ukaguzi unakamilika CAG, alibaini zaidi ya **shilingi bilioni 300** zilikuwa zinahusika katika hoja hii. Taarifa

ya CAG ilibainisha pia, BOT inachukua muda mrefu katika kuharibu fedha chakavu zinazotoka kwenye mzunguko.

2.2.15 Kutokuwepo ufanisi katika Kampuni ya Mzinga (MHCL)

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Mzinga Holding (MHCL) ilianzishwa kama Kampuni tanzu ya Shirika la Mzinga na kusajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni Namba 12 ya Mwaka 2002 (*Companies Act No. 12 of 2002*) mnamo tarehe 23 mwezi Julai mwaka 2010 (*Limited company with limited*).

Mheshimiwa Spika, Dhumuni la uanzishwaji wa Kampuni hii ilikuwa kufanya biashara ili kuongeza mapato ya Shirika. Shughuli za msingi za Kampuni ni pamoja na; ujenzi (*Construction and civil works*), huduma za ushauri wa kitaalamu (*Consultancy services*), kilimo cha kisasa (*Mechanized agriculture*) na shughuli za usafirishaji (*Logistics and distributorship*)

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati pamoja na mahojiano na CAG umebaini kuwa tangu uanzishwaji wa Kampuni hii ufanyike, Kampuni imekuwa ikijikita zaidi katika shughuli ya ujenzi (*Construction & civil works*) bila kutekeleza majukumu mengine kama malengo ya uanzishwaji wake yalivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuwa Kampuni hii imekuwepo kwa miaka takribani kumi, CAG amebaini mapungufu mbalimbali katika uendeshaji wake ikiwa ni pamoja na masuala yafuatayo:-

a) Kampuni tanzu ya Shirika la Mzinga haina uwezo wa kujiendesha yenyewe. Matokeo yake Kampuni imekuwa ikipewa fedha na Shirika kwaajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Kampuni;

b) Kutokuwepo kwa mgawanyo wa uendeshaji na mali kati ya Shirika na Kampuni;

c) Kampuni haina bodi ya Wakurugenzi hadi sasa kinyume na masharti ya uanzishwaji wake;

d) Ofisi ya Kampuni iliyosajiliwa ni katika viwanja vya nane nane lakini Kampuni imekuwa ikitekeleza shughuli zake katika ofisi za Shirika;

e) Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa Kampuni hivyo kusababisha Kampuni kupata hasara katika miradi yake yote; na

f) Kampuni imekuwa ikiendeshwa bila kuwepo Mpango Mkakati (*Corporate strategic plan*).

Mheshimiwa Spika, Dosari za kiutendaji katika Kampuni ya Mzinga zimesababisha miradi mingi ya ujenzi inayotekelezwa na Kampuni hiyo kutokamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya DAS – Ikungi, ujenzi wa wodi ya wanaume katika hospitali ya Wilaya – Nyamagana, ujenzi wa nyumba ya RAS – Singida na ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya- Makambako.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na uwepo wa dosari za kiutendaji, CAG amebaini kuwa, Kampuni ya Mzinga haikuandaa taarifa zake za fedha kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni za Ukaguzi za Kimataifa (*International Audit Standards - IAS*). Mathalani, kwa mwaka 2018/2019 Kampuni ilitoa taarifa kuwa imepata mapato ya **shilingi 9,653,300,158** lakini hapakuwa na uthibitisho wa namna mapato hayo yalivyopatikana.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, CAG hakupata uthibitisho wa namna mapato hayo yalivyopatikana na hivyo kuwa na maoni kwamba taarifa kuhusu mapato hayo sio sahihi na haziakithi taswira sahihi ya Kampuni kinyume na masharti ya ¹⁵Kifungu cha 11 cha Kanuni za Kimataifa za ukaguzi. Aidha, katika kipindi hicho Kampuni imepata hasara ya **shilingi 291,535,504**.

¹⁵ Para 39 and 40 of IAS 11

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya jumla

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2019, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

3.2 Maoni ya jumla

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati yamezingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa, kwa kipindi cha miaka 5 ya uhai wa Bunge la 11, Maazimio ya Bunge kwa Taarifa mbalimbali za Kamati yamekuwa yakifanyiwa kazi na Serikali. Utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwa kiasi kikubwa umesaidia kuongeza nidhamu katika matumizi ya fedha za umma, uwajibikaji na kupunguza mianya ya upotevu wa fedha za umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Taasisi za Serikali kujibu kwa wakati hoja za ukaguzi zinazokuwa zimeibuliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Jambo hili lifanyike sambamba na Serikali kuchukua hatua za Kisheria, kinidhamu na kiuwajibikaji kwa wahusika wanaokuwa wamethibitika kuhusika kwa namna moja au nyingine katika ubadhirifu wa fedha za umma.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika,

matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati ni yale yanayolenga hoja zenye athari ya juu (*High risk issues*) na hivyo kuhitaji utekelezaji wa haraka ili kuondoa matumizi yasiofaa ya fedha za umma katika Taasisi za Serikali. Kwa msingi huo, Kamati inapendekeza maazimio yafuatayo: -

3.3.1 Tathmini ya ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

KWA KUWA, Pamoja na mafanikio na kuongezeka kwa ufanisi wa TRA kwa kipindi cha kati ya mwaka 2010 – 2015, bado kumekuwepo na changamoto kadhaa za kiufanisi katika chombo hicho;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo zinapunguza mapato ya Serikali ambayo yalitakiwa kukusanywa kama kodi;

KWA HIYO BASI, Ili kuongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi, Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali iboreshe hali ya utendaji wa vyombo vinavyotoa maamuzi kuhusu mashauri ya kodi kwa kutenga na kutoa fedha na rasilimali nyinginezo kwa wakati ili kuwezesha uhitimishaji wa mashauri ya kikodi kwa wakati;

b) Serikali iwezeshe TRA kuwa na uwezo wa kushughulikia mashauri ya kikodi na ukusanyaji wa madeni ya kodi na kodi zilizo kadiriwa. Jambo hili litafanikiwa kwa kutenga na kutoa rasilimali za kutosha, uwepo wa watumishi wenye weledi na sifa katika Kitengo cha ukaguzi wa kodi (*Tax audit unit*), Kitengo cha huduma za kitaalam (*Technical services unit*); na Idara ya usimamizi wa madeni ya kodi (*Enforcement and debt management department*);

c) Serikali iimarisha mifumo ya udhibiti katika huduma za utoaji mizigo na ulipaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingizwa ndani ya

Nchi kwa kuhakikisha huduma zote za forodha zinafuatwa ipasavyo ili kuepuka upotevu wa mapato ya Serikali; na

d) Mwisho, Serikali iimarisha udhibiti na ufuatiliaji wa mizigo inayopitia hapa Nchini kwenda Nje ya Nchi (*Transit goods*) ili kuepuka matumizi ya bidhaa hizo katika soko la ndani bila ya kulipiwa kodi.

3.3.2 Malipo yasiyo na manufaa ya shilingi 1,082,301,547 yaliyofanywa na REA

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebaini malipo ya **shilingi 1,082,301,547** yaliyofanywa na REA kwenda kwa Kampuni ya **SMEC INTERNATIONAL PTY LIMITED** hayakuwa na manufaa;

NA KWA KUWA, Kwa kufanya hivyo kumesababisha hasara kwa Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

Serikali ifanye uchunguzi wa kina kuhusu malipo hayo ambayo yana viashiria vya ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka na kuchukua hatua stahiki.

3.3.3 Usimamizi wa mikataba na ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha dosari kadhaa katika usimamizi wa mikataba katika TPA;

NA KWA KUWA, Dosari hizo zimekuwa zikichangia kupunguza ufanisi wa TPA na upotevu wa mapato ya Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) TPA itekeleze kwa ukamilifu matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake katika eneo la usimamizi wa mikataba;

b) CAG kwa mamlaka yake ya Kikatiba na Kisheria aendelee na zoezi la ukaguzi maalum katika eneo la manunuzi, usimikaji na utendaji wa mifumo mbalimbali ya TPA. Aidha, Serikali izingatie mapendekezo ya ukaguzi huo maalum pindi utakapokamilika ili kuboresha shughuli za TPA.

3.3.4 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

KWA KUWA, Kamati imebainisha mapungufu katika usimamizi wa malighafi za utengenezaji wa Vitambulisho vya Taifa na pia kutokuwepo kwa mikataba kati ya NIDA na taasisi mbalimbali zinazotumia taarifa za NIDA;

NA KWA KUWA, Kutokuwepo kwa utaratibu bora wa kuhifadhi malighafi kunaathiri utambuzi wa kufahamu kiasi cha malighafi zilizo salia ghalani ili kupanga mahitaji halisi na pia kutokuwepo mikataba na watumiaji wa taarifa za NIDA kunaipotezea Serikali mapato;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) NIDA iimarisha Udhhibiti wa ndani kwa kuwa na kumbukumbu sahihi za mahitaji halisi ya malighafi ili kufanya manunuzi kwa kuzingatia mahitaji halisi kwa kipindi kifupi; na

b) NIDA iingie mikataba na taasisi zote zinazotumia taarifa zake ili kuongeza mapato ya Serikali na udhibiti wa taarifa za Serikali.

3.3.5 Madeni ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

KWA KUWA, Kamati imechambua na kubainisha uwepo wa deni la jumla ya **shilingi bilioni 454.4** ambalo TANESCO inadai kwa wateja binafsi na taasisi mbalimbali za Serikali;

NA KWA KUWA, Uwepo wa deni hilo unaathiri hali ya utendaji wa kila siku wa TANESCO na unaharibu taswira halisi ya taarifa za hesabu za Shirika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Menejimenti ya TANESCO iimarishe mikakati ya ukusanyaji wa madeni ili kuhakikisha madeni husika yanakusanywa kwa wakati; na

b) Serikali ichukue jitihada mahsusi za kibajeti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinazodaiwa na TANESCO zinalipa madeni yao kwa kuzingatia utaratibu wa kibajeti utakaowekwa na Hazina.

3.3.6 Ukaguzi maalum wa Kampuni ya Pride Tanzania

KWA KUWA, Ukaguzi maalum uliofanywa na CAG umebaini na kuthibitisha matumizi mabaya ya fedha za umma katika Kampuni ya Pride Tanzania;

NA KWA KUWA, Matumizi hayo yanakiuka Sheria za Nchi na yana viasharia vya ubadhirifu wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na CAG katika ukaguzi maalum wa Kampuni ya Pride ili kuendelea kuimarisha udhibiti na uwajibikaji katika fedha za umma.

3.3.7 Matumizi ya shilingi 1,511,995,098 katika Wizara ya Maliasili na Utalii

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imethibitisha matumizi ya **shilingi 1,511,995,098** katika fungu 69 Wizara ya Maliasili na Utalii;

NA KWA KUWA, Matumizi hayo yalifanyika bila ya kuwa kwenye mpango wa bajeti wa Wizara na kabla ya kupata vibali stahiki;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Wizara ya Maliasili na Utalii izingatie kwa ukamilifu matakwa ya Sheria na Kanuni za fedha za umma. Aidha, Wizara ihakikishe shughuli zinazotekelezwa ziwe zimekasimiwa kwenye bajeti ya mwaka husika; na

b) CAG kwa Mamlaka yake ya Kikatiba na Kisheria aendelee na ukaguzi maalum anaofanya kuhusu utaratibu uliotumika

kukusanya fedha hizo, matumizi yake na tathmini ya faida iliyopatikana kwa matumizi husika.

3.3.8 Hali ya kifedha ya Benki za Serikali

KWA KUWA, Taarifa ya CAG pamoja na uchambuzi wa Kamati umebainisha hali ya mtaji wa Benki ya Uwekezaji (Biashara) na Benki ya Uwekezaji (Maendeleo) siyo ya kuridhisha;

NA KWA KUWA, Hali hiyo inakwamisha ufanisi wa Benki kiutendaji na pia unaweza kuisababishia Serikali hasara endapo BOT itazipa adhabu Benki husika;

KWA HIYO BASI, Serikali ifanye tathmini ya mwenendo wa Benki hizo mbili Benki ya Uwekezaji (Biashara) na Benki ya Uwekezaji (Maendeleo), ipitie na kuchambua kwa kina viwango vya mitaji kwa malengo ya kuziongezea mtaji ili ufikie uwiano wa kiwango cha chini cha mitaji kinachotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Benki za Mwaka 2014 au kuzirekebisha kwa kuziunganisha kuunda Benki mpya yenye mtaji wa kutosha (*Restructuring*).

3.3.9 Tathmini ya hali halisi ya mfuko wa PSSSF

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa zoezi la tathmini ya hali halisi ya mfuko wa PSSSF kutekeleza majukumu yake ya baadaye haijafanyika (*Actuarial valuation*);

NA KWA KUWA, Kutofanyika kwa zoezi hilo muhimu kunaikoshesha PSSSF nafasi ya kutambua uwezo wake wa kulipa mafao na uwekezaji kwa siku zijazo;

KWA HIYO BASI, Bodi ya PSSSF ihakikishe kabla ya kufikia mwezi Septemba 2020, zoezi hilo muhimu (*Sensitive and imperative*) linakamilika.

3.3.10 Kampuni ya Mzinga Holding company (MHCL)

KWA KUWA, Kamati imechambua na kubainisha hali isiyoridhisha ya utendaji wa Kampuni ya *Mzinga Holding*

Company ikiwa ni pamoja na Kampuni kupata hasara mfululizo na kutokuwa na mifumo thabiti ya kiutendaji;

NA KWA KUWA, Mapungufu katika uendeshaji yamesababisha Kampuni kutokuwa na ufanisi kiutendaji;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Shirika la Mzinga lifanye mapitio ya Mpango Mkakati wake, ili kutathmini iwapo Kampuni tanzu ya *Mzinga Holding Company* iendelee kutekeleza majukumu yake kwa muundo wa sasa au ivunjwe na kuunganishwa na Shirika mama kwani shughuli zao zinashabihana. Hii itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na kwa kuunganisha nguvu, ufanisi utaongezeka.

3.3.11 Kampuni ya STAMIGOLD

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa Kampuni ya STAMIGOLD imepata hati mbaya ya ukaguzi (*Adverse audit opinion*) kutokana na dosari mbalimbali ikiwamo hali mbaya ya mtaji wa Kampuni na taarifa za fedha zisizo;

NA KWA KUWA, Mapungufu husika yanasababisha Kampuni kupata hasara ambapo kwa mwaka wa ukaguzi 2019 Kampuni ya STAMIGOLD imepata hasara ya **shilingi bilioni 2**;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Madini itekeleze yafuatayo: -

a) Bodi na Menejimenti ya STAMIGOLD wahakikishe wanawasilisha kwa CAG nyaraka zote zinazotakiwa ili uhakiki ufanyike kuhusu madeni mbalimbali ya Kampuni,

b) Serikali kupitia TAKUKURU wakamilishe kwa wakati uchunguzi wa tuhuma mbalimbali unaoendelea katika Kampuni ya STAMIGOLD kwa haraka na kuchukua hatua stahiki; na

c) Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) wahakikishe Kampuni ya STAMIGOLD inapata rasilimali za kutosha kama watumishi wenye sifa, weledi na

wabunifu. Aidha, mtaji wa Kampuni ya STAMIGOLD uongezwe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwa siku zijazo Kampuni hii inasajiliwa katika soko la hisa la Dar es Salaam ili Watanzania wapate fursa ya kumiliki hisa hizo.

3.3.12 Hali ya ukwasi (*liquidity*) katika Bodi za mazao hapa Nchini

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imefafanua kwa kina hali ya ukwasi katika bodi za mazao hapa Nchini kuwa ya kutoridhisha;

NA KWA KUWA, Hali ya kutokuwa na fedha za kutosha inaathiri malengo ya kuanzishwa kwa bodi husika ikiwa ni pamoja na kutosaidia ipasavyo maboresho ya shughuli za kilimo ambacho ndio tegemeo kubwa kwa wananchi kuendesha maisha yao ya kila siku;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Wizara ya Kilimo na bodi za mazao ziboreshe majukumu yaliyokasimiwa kwa bodi za mazao kwa kutekeleza mikakati ambayo inalenga kutatua changamoto za sekta. Jambo hili lifanyike kwa bodi kuwa na mikakati ya kupata rasilimali na kuzielekeza kwenye shughuli za kilimo ili kuwasaidia Wakulima; na

b) Wizara ya Kilimo ifanye tathmini ya kina na ya kitaalamu ili kubaini faida na hasara za uwepo wa bodi nyingi za mazao. Tathmini hiyo isaidie kuangalia uwezekano wa kupunguza baadhi ya bodi kama uwezo wa kuziendesha haupo, ili kuwe na bodi chache zenye majukumu mchanganyiko na zipewe rasilimali za kutosha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

3.3.13 Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kwamba, BOT huchukua muda mrefu katika kuhesabu fedha zinazotoka katika Benki pamoja kuharibu fedha chakavu;

NA KWA KUWA, Kutotekeleza kwa wakati masuala hayo mawili kunaongeza vihatarishi kwa shughuli za kila siku za Benki;

KWA HIYO BASI, BOT iandae mpango na mkakati wa muda mrefu wa kurekebisha dosari hiyo mapema iwezekanavyo.

3.3.14 Kampuni ya Mkulazi Holding

KWA KUWA, Taarifa ya CAG na uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Kampuni ya Mkulazi Holding haijaanza uzalishaji wa sukari kama ilivyokuwa imepangwa hapo awali;

NA KWA KUWA, Kutoanza huko kwa uzalishaji kumesababisha hasara ya takribani shilingi bilioni 8.87 hadi sasa;

KWA HIYO BASI, Kampuni ya Mkulazi itekeleze majukumu yake kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Kampuni ikiwa ni pamoja na kuanza uzalishaji wa sukari katika kipindi cha mwaka 2020-2021 kama walivyomtaarifu CAG. Aidha, Serikali kupitia NSSF ifanye uchambuzi na tathmini ya kina kuhusu mradi huo ili kupata njia bora ya kuutekeleza kwa siku za baadaye, kuepuka kupata hasara na kwa maslahi mapana ya Taifa.

3.3.15 Kutosainiwa kwa hesabu za TTCL na dosari za kiutendaji katika Kampuni hiyo

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa taarifa ya ukaguzi wa hesabu za TTCL haikusainiwa na CAG baada ya kutoridhiwa na Bodi kutokana na hoja zilizokuwa zimetolewa;

NA KWA KUWA, Bodi kutoridhia taarifa hiyo kumeendelea kuathiri hali ya kiutendaji ya TTCL katika eneo la taarifa za hesabu hivyo kutobainisha hali halisi ya ufanisi wa Shirika na kuipotezea Serikali mapato;

KWA HIYO BASI, Serikali ifanye tathmini ya kina ya kiutendaji ya Bodi na Menejimenti ya TTCL (*Management audit*). Kwa kufanya hivyo, Serikali itabaini maeneo ya maboresho ili Kampuni hiyo iendeshwe katika misingi ya utawala bora, ubunifu na ushindani na kuongeza mapato ya Serikali.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, Hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati ya PAC katika kipindi hiki cha uhai wa Bunge la 11. Napenda kutumia fursa hii adhimu na kwa umuhimu wa kipekee kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao kwa miaka hii mitano umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako. Aidha, namshukuru Naibu Spika Mhe. Dr. Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia kuongoza Bunge letu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa uadilifu na weledi mkubwa. Wajumbe hawa kwa kipindi hiki cha miaka mitano wamefanya kazi kwa umoja bila ya kuangalia misimamo ya Vyama na kwa wakati wote waliongozwa na weledi, uzalendo, umoja na maslahi mapana ya Taifa letu. Nawatakia kila lakheri katika mchakato wa uchaguzi unaokuja.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Aeshi Khalfan Hilary, Mb - **Makamu/Mkiti**
3. Mhe. Felister Aloyce Bura, Mb
4. Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa, Mb
5. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb
6. Mhe. Jamal Kassim Ali
7. Mhe. Hussein Abraham Makungu, Mb
8. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb
9. Mhe. Musa Bakari Mbarouk, Mb
10. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb
11. Mhe. Hassan Elias Masala, Mb
12. Mhe. Ignas Aloyce Malocha, Mb
13. Mhe. Ali Salim Khamisi, Mb

14. Mhe. Omar Mohamed Kigua, Mb
15. Mhe. Khadija Nassir Ali, Mb
16. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb
17. Mhe. Maida Hamad Abdallah, Mb
18. Mhe. Josephine Tabitha Chagula, Mb
19. Mhe. Abdallah Haji Ali, Mb
20. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb
21. Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb
22. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb
23. Mhe. Rhoda Edward Kunchela, Mb
24. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
25. Mhe. Joyce Bita Sokombi, Mb
26. Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
27. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati, kupitia kwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Ndugu Wilfred Magova.

Mheshimiwa Spika, Mwisho Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) chini ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu Charles Kichere na shukurani kwa Uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuendelea kuisadia Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake kwa weledi na ufanisi.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI
(PAC)**

22 Mei, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti kwa kusoma hotuba yako ambayo imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge. Hoja hiyo sasa imeshatolewa rasmi, kwa hiyo, tunaendelea na utaratibu.

Kwanza, niwataarifu Waheshimiwa Wabunge ambao wako Msekwa na pia mlioko humu ndani kama kuna Mheshimiwa ambaye angependa kuzungumza siku ya leo basi aniletee jina mapema iwezekanavyo, ndiyo nina-*organise* Meza yangu hapa, ili tuweze kuweka mambo sawasawa. Nasisitiza mapema, siyo ukishasikia wenzio wameongea ndiyo upate mdadi sasa na wewe unataka kuongea. (*Kicheko*)

Ilikuwa Mwenyekiti wa Kamati atuanzishie lakini simuoni na hizi barakoa sijui kama Mheshimiwa Naghenjwa yupo.

MHE. ESTER A. BULAYA: Ana dharura.

SPIKA: *Okay*, hakuna neno, nilikuwa nimepanga tu kichwani kwangu kwamba angeanza kwanza ili atuanzishie zoezi hapa lakini haina shida. Kwa hiyo, tuanze na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Kigua.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema tukaweza kukutana na kuendelea na shughuli za Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia sitoacha kuwashukuru wapigakura wa Jimbo langu la Tanga Mjini ambao kwa kipindi chote cha miaka minne na ushehe hii wamekuwa wakinipa ushirikiano wa hali na mali wa kimwili na kiroho.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati na nitaanzia kwenye malipo ya *REA* ya *1.83 billion*. Kama tumesikia taarifa ni kwamba *REA* walikuwa waweke umeme katika vijiji 1,798 lakini wakamuajiri mhandisi

mshauri (*consultant*) ambaye alikuwa anaandaa taarifa ya kuwasaidia wao kurahisisha kazi yao. Kwa bahati mbaya sasa au tuseme kama ni kwa makusudi, kabla yule *consultant* hajatoa taarifa wenzetu wakaajiri makampuni 27 kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa huyu mhandisi mshauri alilipwa hizi fedha, *1.83 billion*. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali lakini ni ubadhirifu mkubwa wa fedha za Serikali. Pia ukitazama na ukizama kwa ndani pana viashiria vya rushwa. Nishauri tu Serikali kwamba ilianganalie suala hili kwa uzito unaostahili na ikibidi wahusika wachukuliwe hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la vitambulisho vya *NIDA*. Ukitazama suala hili kuna upungufu na makandokando mengi. Kwa mfano, kuna vifaa au *materials* ambazo zimenunuliwa za takribani shilingi bilioni 42, yaani wamenunua *materials* nyingi kuliko mahitaji yaani *material* yatakayotumiwa ni machache lakini wao wamekwishanunua na hayahitajiki. Nayo hii pia ukiangalia ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali na ni ubadhirifu yaani vifaa vimenunuliwa vingi kuliko mahitaji ya *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niishauri Serikali iitupie macho *NIDA* kuna makandokando mengi. Pia ukitazama hata hayo *material* yalinyonunuliwa, wakati wana mtambo wa zamani wamenunua mtambo mwingine mpya, sasa hii *raw material* iliyonunuliwa ya mtambo wa zamani haifanyi kazi kwenye huu mtambo mpya. Vilevile pia hii nayo ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nalotaka kuzungumzia ni suala zima la *PRDE*. *PRIDE* ina mambo mengi na kuna uchafu mwingi humo ndani. Kwa mfano, wakati wanafanyiwa ukaguzi (*special audit*), imeonekana pana ubadhirifu wa takribani shilingi bilioni 10 ambazo zimetumika vibaya. Kama hilo halitoshi, wakati ukaguzi unafanyika wao benki hawakuwa hata na shilingi kumi, hata shilingi moja

hawana. Ina maana walikwenda wakakwapua fedha benki kwa ajili ya kujinufaisha binafsi. Kwa hiyo, hilo nalo naomba lichukuliwe hatua za kinidhamu na Serikali iangalie kwa sababu kuna wajanja wachache walitaka kuifanya *PRIDE* ni kampuni yao binafsi. Sasa hili jambo kwa kweli halikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Wizara ya Maliasili na Utalii, pana matumizi ya *1.5 billion* ambazo zimetumika nje ya bajeti. Ukitazama Kanuni za Fedha, hii ni kinyume na Kanuni ya Fedha ya mwaka 2001 na pia ni ukiukwaji wa Sheria ya Bajeti. Kwa hili, kwanza panahitajika ukaguzi maalum lakini nishauri kwamba hatua zichukuliwe kwa wale wote waliohusika na ubadhirifu huu wa shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, suala zima la *Tanzania Ports Authority* kwa Bandari ya Dar es Salaam. Tumeona kwenye Kamati yetu, kuna mikataba karibu saba ambayo hajiatekelezwa. Vilevile pia hata thamani ya hii miradi saba sisi kama Kamati hatukuweza kuijua. Kama hilo halitoshi, mifumo ya uendeshaji wa shughuli za bandari kwa njia ya kielektroniki bado haijakamilika. Mara zote tumewaita, bahati nzuri nikushukuru umeniteua kuwa Mjumbe wa *PAC* kwa miaka minne, kila tunapowaita Bandari wakija tukiwauliza kuhusu hii mifumo wanatupigapiga chenga, mingine unaambiwa imekamilika, mingine haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme labda wanafanya kwa makusudi kwa sababu kutokamilika kwa hii mifumo ndiyo chanzo kikubwa cha upotevu wa fedha na mapato ya Serikali. Kwa hiyo, naomba Serikali ipaangalie sana Bandari ya Dar es Salaam. Kama tunavyojua bandari ni lango kuu la biashara. Kama sisi hatuwezi kudhibiti mapato yetu ya bandari itakuwa miaka nenda miaka rudi tunapongeza Kenya, Msumbiji (Bandari ya Beira), Durban (Afrika Kusini) na *Port Elizabeth*, wakati sisi nchi nyingi zilizotuzunguka ambazo ni *landlocked countries* wanatumia bandari zetu kwa ukaribu tuliokuwa nao na ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini wenzetu wa bandari mimi nafikiri ama hawajui wajibu

wao au wameweka maslahi yao binafsi mbele. Kwa hiyo, mimi naomba hilo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee vilevile kwenye suala la *Mzinga Holding Company Limited*. Kampuni hii imekuwa inapata hasara mfululizo. Kwa mfano, mwaka jana tu 2019, wmaepata hasara ya milioni 291, sasa inajiendesha kwa hasara. Nashauri kwanza ni vyema hii kampuni ivunjwe irudi kwenye kampuni mama ya Mzinga. Napo hapa ikibidi lazima tuangalie kwamba hii kampuni kwa nini kwanza ilikuwa inajiendesha kwa hasara wakati ni kampuni tuliyoitumaini kwamba itatusaidia sisi katika mazingira yetu haya ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie tu kwa kushukuru ushirikiano ambao Wabunge tumekuwa katika Kamati yetu ya *PAC*. Kama alivyosema Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti hapa kwamba kwenye shughuli za utendaji tumekuwa hatuangalii masuala ya vyama wala hatuangalii huyu anatoka wapi na huyu anatoka wapi, tunashirikiana kama alivyosema kwa njia ya uzalendo lakini lengo ni tutimize jukumu ambalo wewe umetuamini ukatukabidhi la kufanya kazi katika Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile pia nitoe pole kwa wenzetu wale ambao wamepatwa na misukosuko ya kisiasa katika vyama vyao kwa kutolewa nje ya mstari kwa maana ya kufukuzwa. Mimi niseme sisi kama Wapinzani huu siyo muda wa kufukuzana kwa sababu tunaeelekea kwenye uchaguzi ni muda wa kuwa pamoja na kushirikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sisi kama Chama cha Wananchi *CUF* tumewahi kuiongoza hii Kambi Rasmi ya Upinzani karibu mara tatu lakini hatukubagua wenzetu. Kilichojitokeza ambacho sisi sote tumekuwa hatufahamu ni kwamba sisi tumeondolewa hata kwenye Uwaziri Vivuli, hatumo. Mara ya kwanza tukaona labda ni kutokana na mgogoro tuliokuwa nao ndani ya chama lakini hata mgogoro ulipokwisha bado tumewekwa kando katika suala zima la Uwaziri Vivuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwaombe wenzetu, dhambi ya ubaguzi mnapoanza haiishi hapohapo. Sisi wakati huo alianza Mheshimiwa Lwakatare kuongoza hii Kambi, akaja Hamad Rashid, tulikuwa tunashirikiana na vyama vyote. Hata hivyo, katika jambo ambalo sisi *CUF* tumekuwa tukijadiliana mara kwa mara ni hili la wenzetu kututenga, hili jambo sisi halitupendizi hata kidogo. Wakati huo kuna vyama takribani vitano au sita, ilikuwa Mheshimiwa Lwakatare, Mheshimiwa Hamad Rashid wanashirikisha vyama vyote. Sasa wenzetu hili hawalioni kwamba ni tatizo? Tuwaombe tu kwamba...

T A A R I F A

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Tuwaombe tu kwamba suala la ubaguzi ni kama vile kula nyama ya mtu, unapoanza kuwabagua wenzako mwisho mtakuja kubaguana wenyewe kwa wenyewe.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nampa taarifa.

SPIKA: Unapewa taarifa ili umalizie, Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa msemaji, wakati imeundwa Kambi Kivuli hata wa Chama cha Wananchi *CUF* walikuwepo baadaye wao wenyewe wakavurugana. Tukawauliza mnataka muendeleo wakasema *no*, sisi hata hatujulikani kama ni *ACT* au ni Chama cha Wananchi. Tukiwa Mawaziri Vivuli na sisi ni kidogo *ACT* na kidogo *CUF* tutafukuzwa kwenye vyama vyetu. Aseme kama hatukumuuliza? Ni afadhali tuseme ukweli kuliko kuongopa hapa, tunamfurahisha nani? Hiyo ndiyo taarifa yangu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mussa Mbarouk, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo mimi siipokei.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu baada ya kuwa mgogoro umekwisha mahakamani, mimi ndiyo Mwenyekiti wa Wabunge wa *CUF* na nimemfuata mara kadhaa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba wenzangu wamenituma tukae sasa kwa sababu mgogoro umekwisha tuendelee kushirikiana. Mimi niseme tu ndiyo yaleyale kama alivyosema Mwalimu Nyerere, dhambi ya ubaguzi ikianza mtasema wao Wazanzibar sisi Wazanzibara, itakwenda mwisho mtasema wao Wazanzibar sisi Watanganyika, mwisho itakwenda mtageukana kwamba huyu Mchaga, huyu Mnyamwezi, huyu Mdigo, huyu Mbondei, huyu Muhaya.

Mheshimiwa Spika, sasa tuwaombe wenzetu, tuna nia safi kabisa na maneno haya siyo maneno yangu mimi ni maneno ya sisi Wabunge wa *CUF*, kama Mwenyekiti nimetumwa niyaseme kwamba baada ya kutubagua sisi hamuoni sasa na ninyi wenyewe pia mnabaguana? Wakati tunaelekea kwenye uchaguzi kipindi hiki cha kuwa pamoja sisi tunavurugana.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, ujumbe wako umefika. Mheshimiwa Omari Kigua, nakupa robo saa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia kwenye maoni ya Kamati ya *PAC*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maoni yangu juu ya Kamati hii napenda kwa heshima kubwa kabisa nikushukuru wewe kwa kazi kubwa ambayo umeifanya katika kipindi chote hiki ambacho nimekuwepo hapa Bungeni.

Nimetafakari sana nikasema katika kipindi chote hiki ambacho sasa tunamalizia Bunge, toka nimeingia katika Bunge hili nimekuwa Mjumbe wa Kamati hii ya PAC na nimekuwepo hapo kwa sababu uliniamini kuwa Mjumbe wa Kamati hii. Nashukuru sana kwa sababu nimeweza kujifunza mengi sana kupitia Kamati hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, pia ulinipa nafasi ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya Haki, Kinga na Maadili ya Bunge ambayo pia nilitumikia katika kipindi cha miaka miwili na nusu. Kama hiyo haitoshi, ulinipa fursa ya kuwa Mjumbe wa Kamati Maalum ya Kukushauri wewe namna ambavyo Serikali inaweza kufaidika na sekta ya gesi. Nakushukuru sana. Nawaomba Wana-Kongwa wakuchague kwa kura nyingi sana. Unatoshia kwenye nafasi hiyo, lakini nafahamu fika kwamba katika Jimbo lako la Kongwa wako Wana-Kilindi sana ambao mimi nawafahamu, watakupigia kura na wafahamu kwamba unatoshia kwa nafasi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC. Naipongeza sana Serikali, lakini hususan Ofisi ya CAG. Kwa kiasi kikubwa sana Ofisi ya CAG imefanya kazi kubwa sana. Wapo ambao waliamini kwamba baada ya mabadiliko ya CAG mpya pengine taarifa hii isingeeonesha mambo mengi. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii imesheheni mambo mengi sana. Wajibu wetu sisi kama Wajumbe wa Kamati ya PAC na Wabunge wengine ni kuhakikisha kwamba tunakazia yale ambayo CAG ameyazungumza.

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi sana lakini nitajikita maeneo machache sana. Nitaanza na Ofisi ya TRA au Mamlaka ya Mapato. TRA au Ofisi ya Mamlaka ya Mapato ni ofisi ambayo Serikali inaitegemea sana. Ni eneo ambalo Serikali inaendeshwa kutokana na mapato ambayo wenzetu wa TRA wanayasimamia. Ripoti ya CAG ambayo ilifikishwa katika Kamati yetu ilionesha takribani shilingi bilioni 712 hazijaweza kukusanywa na wenzetu wa Mamlaka ya Mapato. Yapo maeneo kwa kweli ukiyaangalia, unaona siyo

kwa sababu tu wenzetu wana udhaifu wa kutokusanya, lakini yalikuwepo maeneo ambayo yalikuwa yanahitaji maamuzi madogo sana.

Mheshimiwa Spika, mfano, Serikali au *TRA* walishindwa kukusanya shilingi bilioni 84.6 kisa tu ni kwamba, Bodi ya Rufaa ya *TRAB* na Bodi ya Rufaa walikuwa wameshindwa kukutana. *Column* ile Wajumbe walishindwa kukutana. Kuna Wajumbe wengine wanatoka Zanzibar; sasa unajuliza, inahitaji *rocket science* kuteua Wajumbe au ile *column* kutimia?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, hususan Waziri mwenye dhamana, Waziri wa Fedha, ahakikishe kwamba bodi hizi zinakutana ili ziweze kutekeleza majukumu yake. Tunaamini kabisa *TRA* wakisimama vizuri wataweza kukusanya maduhuli haya, wataweza kukusanya mapato haya ili miradi ya kimkakati ambayo Serikali inaitekeleza sasa hivi iweze kwenda mbele zaidi. Kiasi hiki ni kingi sana. Naiomba Serikali na nina uhakika kwamba bodi hizi sasa zitaweza kufanya kazi kama ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine katika upande wa *TRA* huo huo ni suala la *tax arrears*. *Tax arrears* ni kiasi kikubwa, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 shilingi bilioni 303 pia zilikuwa hazijakusanywa kwa sababu mbalimbali. Namwomba Waziri mwenye dhamana ya fedha, yupo hapa, ahakikishe kwamba anakutana na wataalam ili pesa hizi ziweze kukusanywa na hoja hizi za ukaguzi ambazo zimejitokeza zisiweze kujitokeza tena.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni juu ya kampuni yetu ya *TTCL*. Kwa kweli, Kamati yako ya *PAC* ilisikitishwa sana na taarifa ya kwamba wenzetu wa *TTCL* wamepata *advice*, wamepata *qualified opinion*, maana yake ni Hati Isiyoridhisha. Kisa ni kwamba, Bodi ya *TTCL* hawakusaini taarifa hii ya *CAG*. Hili jambo halijakaa vizuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, *CAG* anafanya kazi kwa niaba yako wewe. *CAG* ni jicho lako wewe. Tunaamini kabisa

kwamba Serikali inawekeza pesa nyingi sana kwenye makampuni kama haya na ni matarajio wananchi wa Tanzania kwamba *TTCL* ni kampuni mama ambayo ina *upper hand* kubwa sana, lakini ukiiangalia utaona kwamba *shares* zake au nafasi yake katika soko wana asilimia moja tu wakati mkongo wa Taifa wanaumiliki wao *TTCL*.

Mheshimiwa Spika, nini kimetokea hapo? Ni kwamba, Bodi ya *TTCL* hawakusaini hesabu za *CAG* na hiyo ikasababisha *CAG* akatoa *Qualified Opinion*. Sasa jambo hili halileti picha nzuri kwa sababu, pesa hizi ambazo *TTCL* wanazo ni pesa za wananchi wa Tanzania na *CAG* yeye anakagua fedha za wananchi wa Tanzania. Kitendo cha Bodi cha kutoruhusu kusaini taarifa hizi maana yake hawajamtendea haki *CAG*. Siyo kwamba, hawajamtendea *CAG*, ni kwamba hawajalitendea haki Bunge ambalo ndilo linafanya kazi kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Naiomba Serikali katika eneo hili wangalie, Waziri mwenye dhamana ya Ujenzi *TTCL* wako chini yake, aangalie ni kwa nini bodi hii haikupitisha hesabu hizi?

Mheshimiwa Spika, yapo upungufu mwingi, tulipomwuliza Mkaguzi akatuambia, mathalan, katika hesabu ambazo walizileta pale, zilikuwa na changamoto mbalimbali. Mojawapo ni kwamba, ilikuwa inaonekana *TTCL* wanadaiwa na wateja shilingi bilioni 11 ambazo hazina maelezo. Katika uhalisia wa kawaida *TTCL* kudaiwa shilingi bilioni 11 wakati hakuna shughuli yoyote ile ambayo *TTCL* wamepeleka maana yake hizi hesabu zilikuwa zina upungufu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kilichoonekana ni kwamba, *TTCL* wana huduma mbalimbali mikoani, lakini walikuwa wanashindwa kufanya *reconciliation* katika mikoani na walipoulizwa wakawa wanasema kwamba hawana *staff* wa kutosha, mambo ambayo yalikuwa *within management*, wangeweza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la makusanyo ya maduhuli, pia lilikuwa ni eneo ambalo lina changamoto nyingi. Nini maoni yangu kama Mbunge na Mjumbe wa

Kamati ya PAC? Nadhani imefika wakati sasa kwamba, Serikali iangalie na ikae chini na *Management* ya TTCL kuona kwa nini walikataa kusaini taarifa hizi za hesabu? Kitu ambacho kwa kweli, hakijakaa vizuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia na ambalo lilikuja kwenye Kamati yetu ni eneo la PSSF. Ushauri wa CAG ulikuwa ni ushauri mzuri sana; NSSF, LAPF, yalunganishwa na ushauri wa CAG baada ya kuyaunganisha mashirika haya ilikuwa ni kwamba lazima ifanyike tathmini. Kwa nini ilikuwa inafanyika tathmini? Ni kwa sababu mashirika haya yalifanya *investment*; yalifanya uwekezaji kwa kutumia michango ya watumishi. Sasa usipofanya *actual valuation*, maana yake wapo watumishi watakaostaafu ambao hawatapata mafao yao.

Mheshimiwa Spika, kinachotarajiwa hapa ni kwamba, michango ile ambayo watumishi wanatoa, uwekezaji ukifanyika ndiyo itakayolipa mafao ya watumishi wale waliostaafu. Sasa mpaka sasa hivi, mpaka hadi kufikia Aprili 20 *actual valuation* haijafanyika.

Naiomba sana Serikali ifanye *actual valuation* ili tuweze kuwalinda hawa watumishi ambao wameshastaafu. Itafika siku watumishi ambao wamestaafu hawataweza kulipwa mafao yao. Nadhani Serikali ina nafasi kubwa sana ya kupitia na kufanya *actual valuation*.

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike hapa? Kulikuwa na uwekezanji ambao haukuwa na tija. Kwa mfano, Kamati yetu iliona kwamba mifuko hii ilikuwa inawekeza zaidi kwenye kujenga majengo, kitu ambacho hakikuwa sahihi zaidi. Kwa mfano, sasa hivi unaona kabisa kwamba *real estate* imeshuka thamani, majengo thamani yameshuka, hakuna wapangaji Dar es Salaam, hakuna wapangaji Dodoma. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba *investment* katika hii mifuko inakwenda chini. Ipo siku itatokea kwamba watumishi watakosa kulipwa *pension* zao. Nadhani nafasi hiyo ipo, tuipe nafasi Serikali ifanye *valuation*. Namwomba Waziri mwenye dhamana alifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulichangia ni utaratibu ambao wenzetu wa Benki Kuu ya Tanzania huwa wanapokea noti chakavu. Sasa kitu ambacho kimetokea sio cha kawaida ni kwamba benki hizi; *Commercial Bank* na benki nyingine wanapokusanya hizi noti chakavu wanazipeleka Benki Kuu. Sasa Benki Kuu huwa hawahesabu wakati ule ule, wanakaa muda mrefu. Kilichotokea ni kwamba, *CAG* au Mkaguzi aligundua kwamba, takribani shilingi bilioni 300 zilikuwa bado hazijatazamwa kwa maana kwamba, Benki X imeleta Benki Kuu, lakini hawakuangalia kama kuna noti ambazo zimechakaa, kuna noti *fake*, sasa inatokea baada ya miezi sita inaonekana kwamba labda benki fulani imeleta noti ambazo ni *fake* au kwamba, hesabu haziko sawa; Benki Kuu wanatoza *charges*.

Mheshimiwa Spika, sasa hili jambo Kamati imeona kwamba sio zuri. Uwekwe utaratibu kwa wenzetu wa Benki Kuu kwamba wanapopokea hizi noti chakavu wahakikishe kwamba wanazihesabu wakati ule ule ili wasizalishe hoja za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la uwekezaji wa *NSSF* kwenye shamba la sukari la Morogoro hapa. Ni kwamba, *NSSF* walifanya uwekezaji, lakini kilichotokea pale, Serikali ilikuwa na lengo kwamba iwe na mashamba yake ili iweze kuzalisha sukari yenyewe. Sasa kilichotokea bahati mbaya ni kwamba, uamuzi wa kuzalisha sukari wenyewe Tanzania haukufanyika badala yake *management* ile ya shamba waliamua kuuza miwa; na kwa tani moja ilikuwa shilingi 52,000/=, jambo ambalo kwanza Bodi haiku-*approve*, ilikuwa ni *management* ya *NSSF* waliamua tu wao kuuza kwa tani shilingi 52,000/=. Hili halikuwa jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu ni kwamba kuzalisha miwa na kuwa na viwanda vyetu hapa Tanzania ni jambo la msingi kabisa, lakini uamuzi huu uliofanyika haukuwa na tija kwa sababu, pesa zilizotumika ni michango ya wananchi wa Tanzania. Hili lilifanyika na Uongozi wa *NSSF*.

Naishauri Serikali kwamba tunapowekeza tuangalie tunawekeza kwenye nini?

Mheshimiwa Spika, tusiwekeze tu hovyoy kwa sababu, hadi kufikia tarehe za ukaguzi ni kwamba, tayari *NSSF* walikuwa wame-*incur* au shamba hili lilikuwa lime-*incur* gharama ya shilingi bilioni mbili, ni hasara hii. Hizi ni pesa za watumishi, ni michango ya watumishi. naiomba Serikali iangalie tena jambo hili kwa sura nyingine ili uwekezaji huu uwe na tija tuweze kuepuka hasara kama hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kama Mjumbe wa pili katika Kamati ya *PAC*. Nakutakia kila la heri. Nakushukuru sana, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Ruge.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii iliyoko katika Bunge lako Tukufu. Awali ya yote nami nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhudumu kwa kipindi cha miaka miwili na nusu katika Kamati hii nikitokea katika Kamati ya Katiba na Sheria. Nimefarijika sana, nimeweza kujifunza mambo mengi sana. Kwanza kule Katiba na Sheria nimejifunza namna sheria zinavyotungwa, mchakato mzima; zinapoanzia mpaka hatimaye zinakuja hapa Bungeni na hadi mwisho ambapo Mheshimiwa Rais anasaini.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kunipa nafasi ya kwenda katika Kamati hii ya *PAC* kwa ukaguzi wa hesabu za mashirika na Serikali Kuu. Nimejifunza mambo mengi sana tofauti na ambavyo tulikuwa tunasikia, tunaposikia Hati Chafu, Hati yenye Mashaka, Hati Safi, moja kwa moja tulikuwa tu tunadhani ni katika maeneo yale ambayo wakati

mwingine yamegubikwa na ufisadi kumbe kuna taratibu nyingine pia zinahusika katika hizo kaguzi.

Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia katika hoja zetu hizi ambazo ni maazimio karibu 15 ya Kamati yako ya PAC na ningeanza na eneo linalohusu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mamlaka ya Mapato (TRA) bado inaonekana kuna matatizo pamoja na jitihada kubwa ambazo tunazona za kuongezeka kwa wigo wa makusanyo ya kodi, lakini bado kuna maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Eneo mojawapo ambalo CAGameliona ni katika mashauri mengi ya kikodi ambayo hayaamuliwi kwa wakati; takribani shilingi shilingi bilioni 84.6 karibu shilingi bilioni 85 bado hazijafanyiwa maamuzi yoyote, lakini ukichunguza ni kwa namna ambavyo mifumo yake imekuwa haifanyi kazi kwa haraka na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba wenzetu Wizara ya Fedha ambao ndio wanasimamia mamlaka hii kuweka msukumo kuhakikisha kwamba zile Mahakama za Kikodi zifanye kazi kwa wakati na zifanye maamuzi stahiki ili pesa hizi ziweze kufanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, pia, kama ambavyo Kamati yetu imeeleza, kuna *tax arrears* karibia shilingi bilioni 303 nazo hazijakusanywa. Ukija katika uchambuzi utagundua kwamba tunaposema tuna mfumo kwa ujumla, hata rasilimali watu pia ni tatizo. Kwa mfano, karibia nusu ya watumishi katika Idara ya Utawala, kwa maana ya Wakuu wa Idara, nusu yao wote wanafanya kazi kwa ku-*act* kwenye zile nafasi na wako muda mrefu sana hawajawa-*approved* kwenye zile nafasi. Kwa hiyo, moja kwa moja unaona kwamba hili linaweza likasababisha upande mwingine linaleta ufanisi ambao hatuutarajii.

Mheshimiwa Spika, hiyo siyo tu katika ngazi ya Ukuu wa Idara, lakini hata kule mikoani karibia kwenye mikoza zaidi ya sita mameneja wote kule wanakaimu zile nafasi za umeneja. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba mtu anapokuwa anakosa *authoritative* na *administrative management* ya

kuamua na kutenda kwa sababu tu anakaimu, inaweza ikaleta athari katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri mwenye dhamana aangalie eneo hili kwa nini hawa watu wanaendelea kukaimu katika hizo nafasi na ni kwa kipindi cha muda mrefu? Kwa mujibu wa taratibu za utumishi tulitaraji kumwona mtu akikaimu kwa muda usiozidi miezi sita, lakini hapa sasa watu wengine wamezidi zaidi ya mwaka na wengine hata miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningetaka kulizungumzia ni hili la uwekezaji katika shamba la miwa la Mkulazi pamoja na Mbigiri ambao ni ubia kati ya Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) pamoja na Magereza. Uwekezaji huu ni mzuri na ni dhamira njema kabisa ya Serikali hasa katika kuziba lile *gap* la sukari, lakini kinachofanyika pale bado hatujafikia ile dhamira ya Mheshimiwa Rais kutupelekea Tanzania ya viwanda, lakini pia kuhakisha kwamba, hili tatizo la sukari linazidi kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tayari sasa wameshaanza kuvuna miwa, lakini mashine mpaka sasa hivi bado hazijanunuliwa. Ndiyo imesababisha waamue kuuza miwa, kwa sababu, miwa ya sukari haiwezi ikakaa muda mrefu, ina muda maalum ambao lazima ikakamuliwe iweze kuwa sukari. Kwa kuona kwamba hakuna mashine, wameamua sasa kuuza tena kwa bei ndogo, lakini angalao kupunguza hasara.

Mheshimiwa Spika, sasa hili siyo lengo la uanzishwaji wa mradi huu. Mradi huu ulianzishwa makusudi kabisa kwa mahususi kwenda kutatua tatizo la upungufu wa sukari hapa nchini. Kwa hiyo, tunaomba Bunge lako liazimie kabisa kwamba, Serikali imeahidi kabisa kwamba mwaka huu wa fedha 2020/2021 watakwenda kununua mitambo. Kwa hiyo, ni lazima tuweke msisitizo hapa kwamba mitambo inunuliwe ili eneo hili ambalo limekusudiwa kwenda kupunguza shida ya sukari tunaweza kuondoa hilo tatizo.

Mheshimiwa Spika, lingine nichangie katika eneo hili la *Pride Tanzania*. Waheshimiwa Wabunge wengi hapa

watakuwa ni mashahidi hakuna ambaye alikuwa anaamini kwamba hii ni Kampuni ya Serikali. Wengi tulikuwa tunaamini kwamba hii ni sekta binafsi. Hata tulivyokuwa tuna-*google* huko, unaiona kabisa kama ni kampuni binafsi, lakini ukaguzi maalum uliofanywa na CAG pale tumegundua kabisa hii ni kampuni ya Serikali na inatakiwa isimamiwe na *Treasurer*. Msajili wa Hazina lazima asimamie hii Kampuni ya *Pride*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pana ubadhirifu mkubwa sana wa takribani shilingi bilioni 130 ambazo hazionekani zilipo baada ya ukaguzi kufanyika. Tunachoomba Bunge lako Tukufu lielekeze Serikali wote ambao wamehusika katika kampuni hii hatua kali zichukuliwe, pamoja na ubadhirifu wa takribani shilingi bilioni 10 ambazo zimepotea katika mikono ya watumishi na wafanyakazi, basi zote hizi zichukuliwe hatua inavyostahiki.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Mamlaka ya Bandari Tanzania ambapo napo tunafarijika kuona kwamba kuna jitihada kubwa zinazoendelea kwamba angalao shehena ya mizigo imeongezeka katika mwaka 2017/2018 takribani imeongezeka kwa asilimia sita ambapo shehena sasa imefikia karibia uzito wa tani milioni 17, lakini pamoja na kuongezeka kwa shehena, pamoja na jitihada mbalimbali za kuendelea kufanya upanuzi wa bandari ikiwemo ya Mtwara na Tanga, bado mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika bandari hauko vizuri; na hili eneo la kusimika mfumo limechukua muda mrefu takriban sasa tunaenda mwaka wa tano; kila wakati wakija tunazungumza habari hii ya mfumo. Kwa hiyo ningeomba Bunge lako Tukufu lielekeze kabisa na Serikali ihakikishe kwamba eneo hili la kusimika mifumo katika ukusanyaji wa mapato ya bandari na mifumo mingine yote liweze kuchukuliwa kwa uzito unaostahili ili tuweze kupata mapato ambayo tunayakusudia.

Mheshimiwa Spika, bado pia katika eneo la bandari shughuli nyingi zinazohusu manunuzi na mikataba haziko vizuri; kwa hiyo kila mara maeneo ya manunuzi na mikataba yamekuwa ni tatizo. Kwa hiyo tungeomba sana kwamba kwa azimio hili Bunge lako lielekeze Serikali kuhakikisha kwamba

matatizo yote haya ambayo tumeyabaini kupitia Kamati yako ya PAC yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la Shirika la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) ambalo mpaka sasahivi linadai takriban bilioni 454, na sehemu kubwa ya madeni haya ni madeni ya Mashirika ya Umma na Serikali. Tunaiomba sana Serikali ihakikishe kwamba madeni haya yanalipwa; kwa sababu miaka mingi *TANESCO* ilikuwa inafanya vibaya lakini hivi karibuni imeanza kufanya vizuri kiasi kwamba sasa imeanza ku-*break even*.

Mheshimiwa Spika, sasahivi hawapati hasara lakini bado wana madeni makubwa ambayo wanadai Serikali, na madeni mengine ambayo kwakweli hata Serikali tusipowasaidia, watahondwa kuwadai. Kwa mfano kwenye kambi za Jeshi, huwezi kwenda kukata umeme jeshini. Kwanza hata utake, utapita wapi kwenda kukata huo umeme jeshini? Kwa hiyo utaona kabisa kwamba tayari hicho ni kikwazo. Kwa hiyo nimuombe sana Waziri wa Fedha aangalie kama deni hili limeshahakikiwa basi yale yote yanayohusu vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, maeneo yale mahsusi hasa ya kimkakati kama kwenye mitambo ya uzalishaji maji na maeneo mengine yote basi madeni haya yalipwe kwa wakati ili shirika hili ambalo sasa tumeanza kuona linafanya kazi nzuri na limeshaanza kuondoka katika kufanya kazi kwa hasara linaweza kusimama lenyewe.

Mheshimiwa Spika, huo ndio mchango wangu. Nakushukuru sana, naunga mkono hoja ya Kamati katika maazimio yote 15 ya kamati. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi. Nilishakutaja Mheshimiwa Catherine Ruge, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Salim.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hii fursa ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyoko mezani ya Taarifa ya Kamati ya PAC.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi kwenye Shirika la Bandari. Wote tunatambua Shirika la Bandari limekuwa na mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu lakini pia bandari zetu zimekuwa zikihudumia takriban nchi nane, *East Central and Southern part of Africa*. Kwa mantiki hiyo bandari zetu zina *potential and leverage* ya kuweza kuendelea kuongeza mapato ya nchi yetu. Hata hivyo kumekuwa na changamoto kubwa katika Shirika letu la Bandari ambazo naamini zikiweza kufanyiwa kazi kwa wakati zinaweza kuleta tija kwa bandari lakini pia kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ukipitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa miaka mitano utatambua kuwa kuna hoja ambayo imekuwa ikijirudia sana takriban kila mwaka, na hoja hii ni hoja ya mifumo. Mimi nilipata fursa ya kukaa kwenye Kamati ya PAC kwa kipindi cha miaka miwili na niliweza kushuhudia namna ambavyo bandari wamekuwa wanashindwa kukamilisha utekelezaji wa mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato, kulipa pamoja na kuhakikisha taarifa mbalimbali za Shirika la Bandari na Taasisi mbalimbali kama *Bank, TRA*, Bandari Kavu zinaweza kusomana. Ukiangalia kwenye taarifa za CAG kuanzia mwaka 2010 mpaka sasahivi kuna miradi mbalimbali ya TEHAMA ambayo imeanza kutekelezwa lakini kati ya miradi tisa ni miradi mitatu tu ambayo imekamilika. Kwa hiyo kuna miradi tisa ambayo haijakamilika na hivyo kusababisha upotevu wa mapato makubwa kwa bandari na kulia hasara taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuna mfumo mmoja unaitwa *ERP (Enterprise Reporting System)* ulianza kutekelezwa takriban miaka mitano iliyopita lakini mkandarasi ameendelea kulipwa na mpaka sasahivi huu mfumo haujakamilika. Kuna mfumo mwingine unaitwa *Port Operating System*, mfumo huu pia umekuwa ukitekelezwa na wafanyakazi wa ndani wa bandari wakishirikiana na mshauri mwelekezi. Lakini mshauri mwelekezi anaendelea kulipwa tena bila mkataba kinyume kabisa na Sheria ya Manunuzi na kinyume kabisa na utaratibu/ *Financial manual* ya bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpaka tunavyozungumza Shirika la Bandari limeshalipa bilioni 57.5 kwa ajili ya kutekeleza mifumo ya TEHAMA ambayo haijakamilika na haifanyi kazi kwa ufanisi na bado tunaendelea kupoteza mapato mwaka hadi mwaka. Ukiuliza tatizo ni nini hupati majibu. Mimi ninaamini kuna watu ambao wanafaidika na kutokukamilika kwa hii mifumo na ndiyo maana mpaka leo hii mifumo haikamiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tatizo jingine la bandari, kuna tatizo kwenye *management* na nitaeleza kwanini kuna tatizo kwenye *management*. Tangu mwaka 2017 kuna *department* au vitengo mbalimbali vya Bandari vimekuwa *paralyzed* maksudi au kwa bahati mbaya kwa manufaa ya nani, sijui! Ili visiweze kutimiza malengo yake. Kwa mfano, ukiangalia Idara ya TEHAMA kuanzia 2017 imekuwa na *head* mpya kila mwaka; na wa mwisho kabisa aidha kwa kufukuzwa au kwa kuacha kazi, wa mwisho ameacha kazi miezi michache iliyopita na ilitokea kutoelewana na *management*. Sasa kama hakuna *continuity*, hakuna *organization memory*, idara inawezaje kufanya vizuri? Inawezekana hiyo ndiyo ababu hata hii miradi ya TEHAMA inashindwa kuendelea kwa sababu kila siku kuna mtu mpya.

Mheshimiwa Spika, ukienda pia kwenye Idara ya Ukaguzi wa Ndani, idara hii tangu mwaka 2017 pia imekuwa na Wakuu wa Idara wapya kila mwaka. Nitatoa mfano, mwaka 2019 kuna *head* wa *Internal Audit* alikuwa pale, alihamishwa kutoka Makao Makuu ya Bandari na kupelekwa Mpanda. Huyu ni mtu mwenye *CPA*, weledi na ana *PhD*. Sasa unamtoa mtu Makao Makuu wa Bandari ambaye anaweza kuisaidia taasisi anaenda Mpanda kuwa *desk officer*, si bora angepelekwa Taasisi zingine aweze kusaidia Serikali maana haya ni matumizi mabaya ya rasilimaliwatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza Idara ya Ukaguzi wa Ndani ya Bandari, Idara nzima imesimamishwa kazi. Watu zaidi ya 13 wamesimamishwa kazi, sababu ni kupisha ukaguzi wa ndani maalum wa *CAG*. Mimi ninaamini na uzoefu unaonesha kwamba anapokuja Mkaguzi wa

Hesabu za Serikali, Idara ya Ukaguzi wa Ndani ndiyo inatakiwa imsaidie CAG kuweza kufanya ukaguzi wake. Sasa leo hii CAG yuko anafanya ukaguzi maalum, Idara yote ya Ukaguzi wa Ndani iko nyumbani; hana mtu wa kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kuna wakati ilionekana timu ya *Finance* ilienda Bandari ya Kigoma na Bandari ya Mwanza kwenda kufanya ukaguzi wa ndani ilhali kazi ya ukaguzi wa ndani ni kazi ya Idara ya Ukaguzi wa Ndani. Sasa *Finance Department* inaenda kujikagua, hiyo ni *self-review*, hutegemei kupata *impartial opinion* hapo. Kwa hiyo, kuna matatizo ambayo Serikali inabidi kuweka jicho karibu kwenye bandari hasa idara hizi muhimu, Idara ya *TEHAMA*, Ukaguzi wa ndani na kuona kuna shida gani ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nimeona mapendekezo ya Kamati na ninayaunga mkono ya kumtaka CAG afanye *special audit*. Lakini ningependa kushauri kama Idara ya Ukaguzi wa Ndani imeweza kusimamishwa kupisha ukaguzi wa CAG basi naomba Mkurugenzi Mkuu pamoja na *Head of Finance* na wao wasimamishwe kwa muda wapishe ukaguzi ili wasiweze ku-*influence* ukaguzi wa CAG. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kushauri kwenye *TEHAMA*, kwa sababu sasahivi tuna Wakala wa Serikali wa *e-Government* basi apewe hiyo kazi aweze kukamilisha ili tusiweze kuendelea kupoteza mapato ya Serikali kwa kumlipa mkandarasi pesa nyingi ambazo hazina tija na miradi haikamiliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizia kwa hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambapo inaonekana kuna fedha takriban bilioni 1.5 zilitumika bila kufuata utaratibu. Naungana na mapendekezo ya Kamati kwamba kukafanyike *special audit* kuona kwamba kulikuwa na *value for money* ya hizo pesa zilizotumika kwa sababu tunafahamu taratibu za kutumia pesa. Haiwezekani pesa zitumike bila kufuata utaratibu, kwa hiyo hao watu ambao watagundulika walifanya maksudi au hakukuwa na matumizi mazuri ya pesa wakuchukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Catherine Ruge, nilishakutaja Mheshimiwa Ali Salim Khamis.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Spika, Ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na leo hii kuwa hapa Bungeni kwaajili ya kutoa michango yetu na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nikushukuru wewe kwa kunichagua mimi kuwa katika kamati hii ya *PAC* kwa muda wa miaka mitano; nimejifunza vitu vingi kupitia hii Kamati na leo naomba nitoe ushauri wangu kwa Serikali baada ya kufanya uchambuzi wa ripoti hii ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia haya ambayo ameyaaainisha *CAG* mwezi Januari tuliingiza ripoti yetu hapa kwenye Kamati, na kwa kiasi kikubwa mambo mengi humu yameelezwa, Kamati ilieleza matatizo ambayo yapo katika maeneo mbalimbali. Sasa mimi leo nitajikita katika maeneo mawili tu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni eneo la *TTCL*. *TTCL* wamefanya kitendo kimoja cha aibu sana; na kitendo hicho ni aibu kwa sababu *CAG* yuko kwa mamlaka ya Kikatiba lbara ya 143, na *CAG* anapokwenda kufanya ukaguzi anakuwa anashirikiana na Taasisi husika. Kila kitu anachokifanya *CAG* anakirejesha kwao, wanakaa kikao cha pamoja wanakubaliana. Hata hivyo cha kusikitisha *TTCL* wamekataa *opinion* ya mkaguzi jambo ambalo si la kawaida katika utekelezaji wa utawala bora katika Taasisi za umma maana najjuliza ikiwa Rais wa nchi hii amekubali kukaguliwa na *opinion* zote anazopewa na *CAG* amezikubali na leo tunazifanyia kazi kwanini *TTCL* wanamgomea *CAG*?

Mheshimiwa Spika, baada ya kupewa hiyo *opinion* ya hati yenye mashaka kuikataa, *CAG* ameyainisha maeneo ambayo kwanini ilisababisha wao kupata hati ya mashaka

kwa hiyo nitaomba twende kwenye haya mambo ambayo CAG ameyainisha.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo CAG ameliainisha ni utofauti wa kiasi kikubwa cha fedha katika taarifa ya makusanyo katika mifumo wa *TTCL*. Kampuni ina mifumo miwili ya ukusanyaji wa mapato ambao mmoja ni...
Sorry!

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza ambacho Mkaguzi amekionisha ni upungufu wa makusanyo. Billioni 1.75 ambayo amelianisha CAG, *TTCL* hawakuwa na maelezo nayo. Katika vitabu vyao inaonekana kuna fedha hii lakini ukipitia mifumo yao haisomani kwa hiyo kuna upotevu wa mwanzo ambao ameuonesha katiak huu mfumo wa *CVBS* na mfumo huu wa *SUN*. Hilo la kwanza, hiyo ni hoja yake ya kwanza ambayo CAG ameitoa.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja ya pili *TTCL* wameonesha kwamba wanadaiwa bilioni 11 na wateja wa kawaida jambo ambalo sio jambo la kawaida na walipotakiwa kutoa vielelezo juu ya jambo hili hawakuweza kuviwasilisha vielelezo hivi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni upungufu wa *documents* za pesa ambazo wao wamezipokea; bilioni 91.43. Jambo la nne ni kwenye suala la deni. *TTCL* wanasema kwamba wanadai bilioni 6.61 kwa Shirika la *TCRA* lakini *TCRA* wanasema wanadai *TTCL* bilioni 3.87 pekee; na hizi ndiyo zimekuwa *invoice* yaani *TCRA* wameipelekea *invoice* *TTCL* ya *bill* yao ya bilioni 3.87 lakini *TTCL* wanasema wao wanadaiwa bilioni 6.6.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeainishwa ni *balance* ambayo si jambo la kawaida ya bilioni 1.4 ambayo hii pia nayo *TTCL* wameshindwa kutoa *documents* ili kumridhisha mkaguzi katika ukaguzi wake.

Mhesimiwa Spika, na jambo la mwisho ni bilioni 5.9 ambazo ziko katika akaunti ya *payable balance* ambayo pia *TTCL* wameshindwa kutoa maelezo kwa *CAG* na ndiyo maana *CAG* akapeleka hati yenye mashaka.

Mheshimiwa Spika, ukizifanyia hesabu hizi fedha ambazo nimezitaja hapa ambazo *TTCL* imeitia hasara Serikali ya bilioni 115.01. Sasa, ikiwa leo taasisi hii inadiriki kufanya jeuri kama hii na bado wapo sasa ninachoishauri Serikali kwamba hatua sahihi na stahiki zichukuliwe kwa wahusika kwa kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 143 ambayo imemruhusu *CAG* kufanya ukaguzi katika Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili na la mwisho ambalo naomba nichangie ni kuhusu Benki Kuu. Kwakweli Benki Kuu wakati mkaguzi amekwenda amekuta kuna bilioni 300 pesa chakavu ambazo benki za biashara zimepeleleka fedha hizi kama pesa chakavu lakini *BOT* hawakuzikagua hizi fedha wala hawakuzihesabu wala hawakuziangalia baada ya muda kupita ndiyo wamekuja kuzipitai hizi noti ambazo Benki Kuu wanasema wamepewa na Benki za Biashara ni pesa *fake*; inawezekana vipi?

Mheshimiwa Spika, halafu ni utaratibu gani ikiwa leo tu wewe mtu wa kawaida unakwenda benki unachukua au unaweka fedha zako unaziangalia kwanza kwamba ni sahihi ama siyo sahihi ndiyo unaweza kuondoka. Leo Benki Kuu inakaa na bilioni 300 halafu kibaya zaidi, baada ya kusema hayo maana yake wanatoa na *penalty* kupitia haya mabenzi wakati wao fedha hizi hawakuzikagua, wamekaa kwa muda walioona wao unawafaa halafu baadaye wanakwenda kuya-*penalty* mabenzi ya biashara.

Mheshimiwa Spika, jambo hili halina tofati na lile ambalo Benki Kuu ililifanya kuchukua fedha kupitia *Bureau De Change*, wameshaka nazo fedha hizi zaidi ya miaka miwili sasa, hadi leo hii usuluhishi wa jambo hili haujapatikana. *Bureau De Change* zote zimefunguliwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za Benki Kuu; kama kuna tatizo hawa watu

wamelifanya, wapelekwe mahakamani ili mahakama ziamue hawa watu waweze kutafuta maisha mengine ili yaendelee, lakini fedha zao umezuia, huwapi fedha zao, biashara hawafanyi; haiwezekani jambo kama hili, lazima tuone umuhimu. Kama ikiwa hawa watu wamefanya uhalifu, wameifanyia ubadhirifu Serikali, hatua za kisheria zichukuliwe lakini leo unakaa na pesa za watu miaka miwili, hawa watu hawapati pesa zao, wanahangaika na hiyo ndiyo mitaji yao ya kibiashara; hii siyo sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue jambo hili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nafikiri sasa umefika wakati tatizo hili liondoke ili ijulikane kama watu hawa wana matatizo ya kisheria, kama ni kodi walikuwa hawalipi, walipe kodi inayostahiki, lakini kile ambacho kimebaki warejeshewe wenyewe ili waendeleo na maisha yao ya kawaida kwa sababu hawa ni Watanzania na wana familia kama sisi ambavyo tunazo ili waweze kuendelea na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA:Ahsante sana Mheshimiwa Ali Salim Khamis. Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na nitumie nafasi hii kukupongeza kwa kazi nzuri katika mihimili hii ambayo umeitendea haki. Umekuwa na maono makubwa katika Bunge letu na Bunge letu limekuwa Bunge la mfano.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwamba pia amekuwa na maono makubwa kiasi kwamba Waafrika tulikuwa tunadharauliwa na tulikuwa tunadharaulika kwa nchi za wenzetu, lakini wameona maono ya Mheshimiwa Rais, hata ile *lockdown* aliyoacha kuwafungia Watanzania imewasaidia Watanzania kujikwamua kiuchumi. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa jitihada hizo na kwa maono makubwa ambayo Watanzania tunayaona.

Mheshimiwa Spika, lengo la Mheshimiwa Rais kufufua mashirika ya umma yaliyotaka kufa na hasa mashirika kama *TTCL* na mashirika mengine ni kuongeza huduma kwa Watanzania. Suala la Kampuni ya Simu limezungumzwa na tumeona mambo ya ajabu sana katika Kampuni ya *TTCL*. Kwa hali ilivyo sasa hivi *TTCL* haiwezi kushindana na Makampuni ya Simu kama *Tigo*, *Airtel*, *Vodacom* na mengineyo kwa sababu kuna madeni ya ajabu pale; shirika haliwezi kudaiwa bilioni 11 na wateja kwa jambo gani, bilioni 11 na wateja. Kwa hiyo ni mambo ambayo hata Mheshimiwa Rais aliyewapa jukumu la kuendesha lile shirika atashangaa kusikia mambo haya. Kuna madeni yasiyoelweka, Waheshimiwa Wabunge wameeleza, sitaki kueleza kwa undani zaidi kwa sababu ipo kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naliona ni muhimu tulizungumzie, Wizara na taasisi zote tunapanga bajeti kila mwaka. Kipindi hiki tupo katika kipindi cha bajeti na kila Wizara na taasisi imepangiwa bajeti yake, lakini kuna madeni yasiyolipika, madeni yaliyopo yanaweza kuiua *TANESCO*, ingawa wanafanya vizuri. Kuna madeni ya bilioni 454, madeni haya ni ya taasisi za umma na Idara za Serikali na madeni mengine ni kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, niombe sasa *TANESCO* na Wizara husika, *TANESCO* wakusanye haya madeni, wanafanya vizuri na tangu Awamu ya Tano iingie ukataji wa umeme siuni sana, kama umeme unakatika ni mara chache sana. Kwa hiyo, ni utendaji mzuri unaoendelea, lakini wasaidiwe kukusanya madeni.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Rais alisema kwamba kuna taasisi inayodaiwa kuna maneno manne tu 'kata', sasa sijui hii 'kata' imeishia wapi. Wanadai madeni makubwa na madeni haya yanaweza kuathiri financial *statement* ya *TANESCO*. Kwa hiyo, niwaombe watu wa Wizara wasaidiane na *TANESCO* na Wizara ya Fedha tuwasaidie *TANESCO* kukusanya madeni haya, bilioni 454 ni fedha nyingi sana na hizi fedha zingepelikwa kule *Stiegler's Gorge* zingefanya kazi kubwa

kuliko ilivyo sasa hivi; zingesogeza shughuli zinazofanyika pale kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, tuna suala la shilingi bilioni 1.5 zilizotumika na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya shughuli za utalii lakini kama tunavyoelewa kwamba kila kitu kinachotendeka ndani ya Serikali yetu lazima ipite kwenye Bunge lako Tukufu na lazima Wabunge waridhie ndiyo fedha hizo zitumike. Kiasi hiki cha bilioni 1.5 hakikuidhinishwa na Bunge na kibali walichopata walikipata baada ya matumizi. Nadhani kama kuna haraka ya matumizi wangeomba kibali cha matumizi wakapata kibali kabla hawajatumia hizi fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo inaelekea kwamba hizi fedha kama *CAG* alivyotoa taarifa kwamba zilitumika hata kabla ya kibali kutoka. Niombe Wizara na wasimamizi wa Wizara kwamba wafuate taratibu, kanuni na sheria za fedha ili lawama isiwepo na matatizo haya yanayoonekana kwenye vitabu vyao visionekane tena.

Mheshimiwa Spika, *Pride* Tanzania ilianzishwa mwaka 1988 na hisa iliyoanzisha *Pride* Tanzania ni fedha za Serikali kwa asilimia 100. Mwaka 2016 *Ernest and Young* walikagua *Pride* Tanzania wakakuta kwamba *Pride* Tanzania ina shilingi milioni 428 lakini ukaguzi maalum wa *CAG* ulipokagua *Pride* Tanzania kulikuwa hakuna salio, yaani baada ya miaka mitatu hivi hakuna salio. Kwa hiyo, ni jambo la kuhuzunisha kwa sababu hizi fedha ni za umma asilimia mia, lakini baada ya miaka mitatu fedha hazikuonekana. *Pride* Tanzania wakasema kwamba walinunua dhamana *CRDB* shilingi bilioni 29 na wakanunua dhamana Benki *M* na kwenye taasisi mbalimbali za kifedha, lakini baadaye ilikuja kugundulika kwamba fedha zile walizokuwa wametolea taarifa zilikuwa fedha kwa ajili ya kulipa madeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *CAG* walipokwenda *Azania Bank* ambao walikuwa wanaiangalia Bank *M* baada ya kuwekwa kwenye uangalizi, wakakuta kwamba hakuna fedha za taasisi hii ya *Pride* Tanzania na wamekuta kwamba bilioni 11,148 wanadaiwa wafanyakazi 168. Hebu chukua

bilioni 11, 148 gawa kwa watumishi 168 kila mmoja katoka na mabilioni mangapi na mpaka sasa hatujajua kwamba ni hatua gani zilizochukuliwa kwa watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *REA* iliingia mkataba na Kampuni ya *SMEC Int. Limited* kama washauri wa kitaalam kwa ajili ya uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa jumla ya shilingi bilioni moja na milioni themanini na tatu lakini kabla hawa hawajatoa taarifa yao, *REA* na *TANESCO* walikwishaajiri wakandarasi 29 kwa ajili ya kufanya kazi kabla ya ripoti ya kampuni hii iliyolipwa bilioni moja na milioni themanini na tatu haijatoa ripoti yake.

Kwa hiyo, hizi fedha bilioni moja ni fedha zisizo na manufaa kwa Taifa letu, ni hasara kwa Taifa kwa sababu wale hawawezi kurudisha fedha na *TANESCO* na *REA* wameajiri makampuni bila kupata ushauri kwa mshauri ambaye walikuwa wamemwajiri. Kwa hiyo, tunaona kwamba hizi fedha zimekwenda bure hazitasaidia Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, pia *CAG* ameona kasoro katika Bodi za Mazao, tuna bodi tisa (9) za mazao, lakini katika bodi hizi tisa (9), bodi tano (5) zinaendeshwa kwa hasara; bodi tano (5) ni sawa na asilimia 56 kati ya bodi zile tisa (9). Kwa hiyo, bodi nne (4) hazina namna ya kujiendesha mpaka zipate ruzuku Serikalini. Kwa hiyo, Kamati yetu inashauri kwamba Serikali ione namna ya kufanya bodi hizi zikajiendesha; tuna Bodi ya Pamba, Bodi ya Korosho, Bodi ya Kahawa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko lakini Bodi ya Mazao Mchanganyiko inafanya vizuri, isipokuwa Bodi ya Kahawa, Bodi ya Korosho na Bodi ya Pamba hazifanyi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kamati inashauri kwamba Serikali ione namna ya kufanya hizi bodi zikajitegemea, zikafanya vizuri kwa sababu mpaka sasa Serikali inajitahidi sana kusaidia Sekta ya Kilimo, Sekta ya Tumbaku, Sukari, Chai, Mkonge, Kahawa na Bodi ya Nafaka Mchanganyiko. Bodi hizi hazijaweza kusimama kwa miguu yake nabado wanategemea fedha kutoka Serikalini kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa muda niliopata, Mungu akubariki, akujalie afya njema na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA:Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura. Mheshimiwa Halima Mdee nakupa dakika 15 atafuata Mheshimiwa Allan Kiula na yeye dakika 15.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mosi na mimi naunga mkono taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ningepomba kwa kuanza niweze kupata *progress* kutoka kwa Waziri wa Fedha juu ya mustakabali wa miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 245 ambayo ilikuwa inafanyika Jimbo la Kawe kwa mantiki ya kwamba mradi 700111 wenye thamani ya shilingi bilioni 142 na mradi 700112 wenye thamani ya shilingi bilioni 102.

Mheshimiwa Spika, inafahamika kwamba mikataba hii iliingiwa mwaka 2017 ikitarajiwa miradi itakamilika mwaka 2019. Samahani mikataba ilisitishwa mwaka 2017 iliingiwa kabla ya hapo kwa maelezo kwamba kuna vitu ambavyo havijakaa sawa. Sasa na kwa mujibu wa ile mikataba ya ujenzi wa haya maeneo mawili *project* nzima zilitarajiwa kukamilika mwaka 2019. Sasa leo tupo mwaka 2020, miradi ya ujenzi wa nyumba imelala, lakini vilevile tunaambiwa kama miradi husika isipokamilika kwa mujibu wa matakwa ya mkataba, Serikali itatakiwa kulipa wakandarasi kama hasara ama kukivunja ama kichumbia cha mkataba shilingi bilioni 99.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa sababu ya hili ziuo na nilizungumza mwezi Januari mwaka huu ni kwa sababu Shirika la Nyumba lilikuwa limefikia ukomo wake wa kukopa wa shilingi bilioni 300. Kwa hiyo, ikatakiwa ipate idhini ya Wizara ya Fedha ili iweze kuongeza mkopo ili miradi husika iendelee, Wizara ya Fedha ipate kipato *through property tax* na mauzo ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, sasa leo mwezi Juni mikataba ilitakiwa iishe 2019, Serikali italipa bilioni 100 za ziada kwa kuvunja mikataba. Mwezi wa kwanza Waziri wa Ardhi na Waziri wa Fedha walisema kuna vitu wana-*review* kwenye mkataba. Sasa ni muhimu kwa kuzingatia wingi wa hii fedha ni muhimu sana tuambiwe baada ya ku-*review* mkataba, sasa tunaendaje mbele. Hai-*make sense* unazuia shirika lisikope hela halafu unakuja kutoa bilioni 100 bure, *it doesn't make sense*. Kwa hiyo, naomba kwa sababu umesema hili ndiyo Bunge letu la mwisho na huu mchakato ulianza kuanzia 2013 mpaka sasa, tuweze kuambiwa hali ikoje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiacha bilioni 99.9, kuna bilioni 2.6 itabidi zirudishwe kwa Watanzania ambao walikuwa wameanza kulipia zile nyumba kwa sababu ilikuwa ni *prime area* na *prime project* kwa hiyo watu walikuwa tayari wameshawekeza fedha zao pale.

Mheshimiwa Spika, nilisema hilo nianze nalo la kwanza ili niweze kupata maelezo mazuri kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kawe wa mwaka wa 10 sasa, ile *project* ilikuwa inabadilisha siyo tu Jimbo la Kawe bali Dar es Salaam kwa kiwango kikubwa sana, lakini zaidi ingesaidia Serikali kupata mapato. Kwa hiyo, tunaomba majibu yenye uhakika kwa kuzingatia tunamaliza muda wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la mifuko ya hifadhi. Mwezi wa kwanza nilisema hivi *CAG* huwa wanatoa taarifa nzuri sana, lakini kuna wakati mwingine sisi hatukielezi kwa bayana kile ambacho *CAG* amekieleza ili Bunge likifanya maazimio, lifanye maazimio yenye tija yatakayoacha heshima ya Bunge, lakini vizuri zaidi kulisaidia Taifa. Nikiangalia taarifa ya Kamati kuhusiana na mifuko na hususan *PSPF* wanazungumzia suala la *actuarial evaluation*.

Mheshimiwa Spika, wakati tunatunga sheria mwaka 2018 kama sikosei au wakati tunaunganisha ile mifuko, tulimuuliza Mheshimiwa Jenister Mhagama hapa kwamba tunajua mnaunganisha hii mifuko baada ya kukopa pesa za mifuko ambayo ni michango ya wanachama, hamlipi ili

kuficha kichocho mmeamua muunganishe hii mifuko ili kuficha aibu ya Mfuko wa PSPF. Tuliwaambia hapa, Mheshimiwa Jenister akasema tunaunganisha tumeshafanya *actuarial evaluation* tunajua mzigo wa madeni na uwezo wa kulipa mafao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati haijieleza kabisa alichozungumzia CAG; CAG amesema Serikali mnadaiwa na hii mifuko kwa sababu kuunganisha mifuko hakuondoi pesa za wananchi mlizozichukua, yaani msijemkafikiria eti mmeunganisha mifuko kwa sababu zile pesa siyo zenu, ni za Watanzania mmojammoja wanaokusanya hela kwenye mfuko wa hifadhi ili wakizeeka waweze kupata pensheni, wakipata ajali kazini na wakiumwa waweze kupata mafao ya kuumwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inadaiwa shilingi trilioni 2.417, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kujumla wake wanadai trilioni 1.466 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma milioni 731 mfuko wa Bima ya Afya shilingi bilioni 220 hapa kwenye taarifa ya kamati hatuzungumzii kabisa juu ya pesa za wananchi ambazo Serikali mlikopa mnatakiwa mlipe. Ukikopa usipolipa hauna tofauti na mwizi wa kuaminiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikichukua milioni 50 kwako ukinidai halafu nazunguka zunguka, mimi ni mwizi tu wa kuaminiwa. Kwa hiyo, naomba sana

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: taarifa iko Msekwa iko wapi? Hapa hapa ndani Mheshimiwa Kigua.

T A A R I F A

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwanza siyo *actual evaluation* ni *actual valuation* moja.

MBUNGE FULANI: Taarifa ni moja tu!

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, lakini la pili suala la kufanya *actual valuation essence* yake ni pamoja kujua kiasi cha madeni unayodaiwa madeni unayodai kwa hiyo, yote hayo yapo katika sehemu ya ripoti. Nadhani mzungumzaji siyo sahihi ku-*challenge* taarifa ya CAG au taarifa ya kamati, ahsante.

SPIKA: Unapokea hiyo taarifa Mheshimiwa Halima?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nasema hivi madeni yanayodaiwa Serikali kutoka kwenye mifuko ya Hifadhi ya Jamii inajulikana siyo mwaka wa kwanza zaidi ya miaka 10 madeni yanajulikana ndiyo maana hapa ni hii ripoti ya CAG ya mwaka 2017/2018 imeandikwa ripoti ya CAG tunayojadili sasa ya mwaka 2018/2019 imeandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja hapa Serikali inatakiwa ituambie italipa lini, halafu kingine unakumbuka uzuri sisi maseneta huku tunajua kabla ya wastaafu au kabla ya mwaka 1999 wakati huo wao walikuwa hawachangii mfuko wa PSPF ukapewa mzigo kwamba jamani kuanzia 1999 kwenda mbele wanachangia kuna wastaafu ambao walikuwa kazini 1999 kurudi nyuma walipeni sisi Serikali tutalipia.

Mheshimiwa Spika, CAG wamezungumza zaidi ya trilioni 11 PSPF wanalipa watu waliostaafu Serikali hailipi sasa nataka Waziri wa Fedha akija hapa akichangia kama sisi wengine tunaochangia waelezee yale madeni ya mfuko kabla ya mwaka 1999 wale watumishi yanalipwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CAG amesema hapa *clear* mifuko ukurasa wa 132 kwamba mifuko iko katika hali ya ukata kiasi cha kukwaza utekelezaji wa majukumu yake. Hii ni kauli ya CAG mpya wala siyo wa zamani, sasa mnakopaje hamlipi? Ndiyo maana sasa hivi wastaafu kulipwa ni *challenge*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango nashukuru uko hapa ukienda kwenye utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya mwaka huu ukienda *item* namba 2 inazungumzia *commitment* ya Serikali iliyoifanya tarehe 15 Desemba, 2015 kupitia barua namba CAA.452/479/01 kwamba watabadilisha mkopo husika kuwa hati fungani. 2015 *commitment* sawa! Hatuwezi kulipa *cash* tunabadilisha kuwa hati fungani na utaratibu wa hati fungani unajulikana CAG anasema leo hawa Waheshimiwa hapa kwanza hawajatekeleza kabisa ile *commitment* yao 2015, pili wameendelea kuchukua pesa za watazania masikini bila hata mikataba. Yaani wazazi wetu wanachanga wapiga kura wetu wanachanga ili wakipata majanga fedha zivasaidie nyie mnachukua hakuna hata mkataba wa maandikiano ndiyo maana tukija kuwadai mnaanza kujifanya tufanye uhakiki unahakiki nini wakati hakuna mkataba ambao unaainisha kwamba umechukua nini? Tuache kujivika kilemba kwamba *we care so much...* (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Dkt Ashatu taarifa

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kama hakuna mikataba hizo pesa anazosema zimechukuliwa amejuaje zimechukuliwa na Serikali kama hakuna mikataba? Kwa hiyo, ni vizuri muongeeaji akaji-*confine* kwenye hoja ukisoma taarifa ya PAC iliyowasilishwa mbele yako hoja anazoziongea hazipo. Kwa hiyo, ni muhimu sana turudi kwenye hoja ni kipi tunachokiongea. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Halima taarifa hiyo!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, tofauti ya maseneta na manjuka kwa lugha ya *form one* ndiyo hiyo

njuka ni mtu mgeni mimi ni *senator*. Hapa tunajadili taarifa za mifuko na rejea *CAG* amezungumzia nini kuhusiana na mifuko tuna tatizo kubwa la deni na rejea *CAG* amesema hapa nimekupa rejea ukurasa wa 291 ripoti tunayojadili sasa mliji-*commit* kwa barua nimewapa *reference number* mkatafute *reference number* huko ofisini kwenu baada ya hapo *CAG* anasema mnachukua pesa zetu bila makubaliano ya kisheria maana yake huo nimerudia ni wizi wa kuaminiwa kalipeni fedha za watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la *UDA* unakumbuka na kwa hili nitoe pongezi kwa *CAG* huyu wa sasa ambaye amekwenda kufanya ukaguzi maalum wa Shirika la *UDA* mungu anajua hili shirika tokea mwaka 2013 wakati ule Jiji lilipokuwa chini ya *CCM* waliingia mkataba wa kuuza *UDA* kwa kipande cha pipi tukawaambia *Simon Group* hana uwezo wa kununua shirika alichukua mali za *UDA* akatumia kama dhamana ya mkopo wa kwenda kulipia tena *UDA* tukaja tukazungumza hapa Serikali ikasema lile dili lilikuwa sahihi. Miaka 6 baadaye na mnakumbuka tukawa ilivyochukua Jiji kikao chetu cha kwanza tukabatilisha mauziano ya *UDA* tukasema kuna ufasidi wa hali ya juu kwasababu mkataba ulikuwa umejaa rushwa na yenye uchafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *CAG* leo anasema kampuni ya *Simon Group* ilinunua hisa za *UDA* na kufanya malipo kwa kutumia njia za udanganyifu. Tafsiri yake ni nini, tafsiri yake ni kwamba tuitake Serikali leo ituambie mustakabali wa hisa za *UDA* za iliyokuwa ama iliyokuwa halmashauri ya Jiji tunaomba leo kwasababu *CAG* amezungumza mchakato wa mauziano ya hisa ulikuwa batili mosi msajili wa Hazina hakushirikishwa, pili Waziri Mkuu kipindi kile ambaye ndiye alikuwa kiongozi mkuu wa *TAMISEMI* na sasa hivi Rais Dkt. Magufuli ambaye ndiye Waziri wa *TAMISEMI* kipindi kile Mheshimiwa Pinda hakuidhinisha yale mauziano ya hisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwenyekiti hili jambo bahati mbaya sana ndiyo juzi lilimuondoa Meya wetu wa Jiji kwanini kwasababu *CHADEMA* na *UKAWA* tulisema hatuwezi

kuruhusu kutumia milioni 5 za wizi wanasema tunakufukuza kwasababu

SPIKA: malizia kwa dakika moja dakika zako zimeisha

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kidogo nashukuru naomba Serikali hili suala liangaliwe na Meya wetu alisimama kidete kulinda maslahi ya Umma akasema hatuwezi kutumia bilioni 5 ambazo ni chafu. Madiwani wa CCM ambao walikuwa wachache kwa kushirikiana nitasema na Waziri wa TAMISEMI, sababu tulikata rufaa kwake hajajibu wakamuengua. Leo CAG anasema ule ulikuwa ni wizi mtupu kwahiyo nataka majibu ya Serikali kuhusiana na UDA na itakuwa ni uungwana mkimuomba radhi Meya wa Jiji aliyegomea kutumia hizi pesa mkasema ati kutokutumia kwake ni kutokutekeleza ama kutumia mamlaka yake vibaya. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, sana. (Makofi/Vigelegele)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee ahsante sana Mheshimiwa Allan Kiula una robo saa atafata Mheshimiwa Rhoda Kunchela

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bunge letu la mwisho na pia PAC kupata nafasi ya kuwasilisha ripoti kwa utaratibu huu ambao uliona ni vema iwasilishwe kwa utaratibu huu kwasababu huwa tunawasilisha ripoti ya mwaka. Lakini sasa baada ya CAG kuwasilisha ripoti leo umetupa nafasi ya kuwasilisha ripoti na hii inaonyesha umakini wako na nia yako ya dhati ya kuweza kuisaidia Serikali kwamba kabla Bunge halijafikia ukomo wake basi uwe umeisaidia Serikali. Wenzangu wamesema maneno mengi kwamba wewe ni Spika wa mfano na wote wanaosimama hapa wanakuombea heri na wanakuombea baraka kwasababu umelitoa Bunge hili mahali fulani na umelifikisha

mahali pa juu. Kwa hiyo mwenyezi mungu akubariki sana.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye hoja au ripoti ya kamati. Kwenye utangulizi imeonyesha kwamba tumeweza kukutana na mashirika mangapi ya Serikali mashirika ya umma lakini na Serikali Kuu tumetoa ripoti hapa na mambo hayo ndiyo yalizalisha ule mchango au mashauri 14 ambayo maazimio ambayo Bunge linapendekezwa lishauri na haya yaliyoandikwa tuliona sisi ni mambo ya msingi kabisa na ni mambo makubwa kwa bahati nzuri niliwahi kufanyakazi *NSSF* nilipenda kuanzia kwenye *PSSSF* nikianzia kwa kufanya kazi *NSSF* na uzoefu wa *social security schemes* mifuko ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, jambo moja ambalo inabidi tuliweke wazi ni kwamba kamati imesema ifanyike *actuarial valuation, actuarial valuation* itaonyesha hali ya mfuko pamoja na kuona mfuko uko vipi kwasababu wote tunajua kusoma namba kwa hiyo, ile itatoa dira na ikitoa dira Serikali itaona sasa ichukue hatua gani.

Mheshimiwa Spika, lakini nikirudi nyuma kwenye kuunganisha mifuko, kwa wasiofahamu Serikali ilipoamua kuunganisha mifuko kila mifuko ilikuwa na wanachama wake na kazi ya mifuko ya hifadhi ya jamii kuandikisha wanachama kusajili kukusanya michango kuwekeza na kulipa mafao. Sasa kila mfuko ulikuwa na wanachama wake na ulikuwa na miradi yake na ulikuwa na mfumo wake na idadi ya mafao tofauti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapokuja kuunganisha mifuko lazima hivyo vitu vyote wange *take into consideration* hizo hatua zote ndiyo maana moja ya jambo lililofanyika *PSSSF* wako wanachama wametolewa *PSSSF* wakapelekwa *NSSF* na ile ina *burden* yake na inataka *decision* yake ndiyo maana ikifanyika *actuarial valuation* utakuja ushauri na ushauri huo ni pamoja na Serikali kuona ichukue hatua gani ili mfuko huo uweze kuwa na fedha za kutosha lakini uweze kuwa na rasilimali za kutosha kwasababu michango haitoshi kulipia mafao ya wanachama au *risk* zinapokuwa juu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hicho ndicho kamati ilichosema na nasimama hapa kusisitiza kwamba *actuarial valuation* ifanyike ikifanyika ndipo tutakuja na mapendekezo sahihi na Serikali itatoa maamuzi lakini leo hii huwezi kusema pesa walipwe unamlipa nani mifuko imeshakufa kila mtu alikuwa na madeni yake? Kwa hiyo, hilo ndiyo jambo la msingi na mali ziko wapi tujue mali ziko wapi na ni mali za nani na mali zinagawiwa vipi? Huo ndiyo utaratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiwa uko kwenye eneo hilo utajua kitu kipi kinatakiwa kifanyike na mimi nilishakuwa kule kwahiyona nasema kwa *authority* kwamba kilichotakiwa kufanyika ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo la kufanyia *actuarial valuation*, tuje kwenye suala la benki zinazomilikiwa na Serikali tunachosema benki ya uwekezaji maendeleo au benki ya uwekezaji biashara zina-*operate* chini ya mtaji huo ndiyo ujumbe ambao CAG aliuleta na ndiyo ujumbe ambao kamati imeuchukua na tukajiliza maswali kwa nini ina-*operate* chini ya mtaji?

Mheshimiwa Spika, lakini pia tukaona kuna riba kubwa ya mikopo tukaona bado mikopo chechefu ipo na tukashauri sasa hizo benki ifanyike *review* au ziunganishwe lakini pia Serikali iongeze mtaji kwasababu benki hizo hatushauri zivunjwe ukivunja benki hizo zilianzishwa kwa lengo maalum zinatija yake kwa Taifa na Serikali lazima itupie jicho hicho ndicho kamati inachosema na ndicho CAG alichosema kwasababu CAG anatuonyesha *position* ya sasa hivi ya benki hizo ikoje. Ametupa *position* sisi tunatoa ushauri na Bunge linatoa ushauri. Kwa hiyo, bado nasimama na hoja ile ya hoja ya kamati kwamba zifanyiwe *review* au ziunganishwe lakini pia mtaji uweze kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, suala la *TTCL* tumelizungumza sana suala hili limeisikitisha sana kamati na ilifikia wakati tukasema ikaonekana kama tusililete yaani kwamba tusilijadili wajumbe wakasema hapana lazima tujadili kwasababu hesabu zao hazikusainiwa sasa tungejadili vipi na wewe ulishatupa kibali

cha kujadili tukaona lazima tujadili suala hili. Kwa hiyo, bodi ya *TTCL* imefanya jambo ambalo ni *unusual* jambo ambalo siyo la kawaida, ni jambo ambalo Bunge hili linatakiwa litoe azimio kali likemee kitendo hicho lakini kwanini hawakusaini yako mambo mengi lakini mambo mawili ambayo *CAG* aliyazungumza pale ndani kuna madeni ambayo yenyewe inadai bilioni 91 sasa bilioni 91 ukim dai lazima mdaiwa awepo na useme unam dai kwa lipi jambo hilo halikuweza kuelezeka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia yenyewe inadaiwa bilioni 11 sawa huyo anayedai ni nani? Na anadai kwa huduma ipi aliyotoa. Kwa hiyo, tukaona hapo kuna mashaka mengi, tukashauri kwamba lazima zichukuliwe hatua za makusudi ili kuweza kuinusuru *TTCL* na *TTeCL* iweze kusimama kama Shirika la Taifa na liweze kuleta tija kutokusaini hesabu siyo jibu. Jibu ni kutekeleza wajibu uliopewa kwasababu ukipewa wajibu wa kusimamia shirika au bodi kusimamia shirika inatakiwa iweze kusimamia kikamilifu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hoja kubwa ya kamati na ndiyo pendekezo letu liko kule ukurasa wa mwisho tumeomba Bunge liweze kupokea hilo pendekezo.

Mheshimiwa Spika, yako mashirika ambayo ni *center of excellence* mojawapo ni Benki Kuu ya Tanzania yako mambo mengi hilo ni moja tu ambalo lilizungumzwa lakini ukisoma kwenye ripoti ya *CAG* utakutana na mengine yapo mle ndani ingawaje zile noti siyo *expense* lakini zile noti zina maana yake kwanini zinarudishwa sasa zinatakiwa zitambulike ziwe *counted*.

Mheshimiwa Spika, ujazi wa fedha kwenye mfumo, kwenye mzunguko unakuwa *determine* na zile zilizotolewa. Kwa hiyo, ni hoja kubwa na ya msingi. Kama hiyo ni *centre of excellence*, kwa nini *BoT* inaruhusu jambo kama hilo? Kuna wasomi wa kila aina.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilivyomaliza Chuo Kikuu niliomba pale, siku pata *First Class*, walikuwa wanachukua watu wa *First Class*. Hasa pale wamejaa watu wa *First Class* tu, lakini hiyo ni moja ya *process* ndani ya Benki Kuu. Kwa nini haifanyiki kikamilifu? Kwa hiyo, jambo hilo na

lenyewe ni muhimu likaweza kuangaliwa na Benki Kuu yenyewe ikajiangalia kwamba unaweza ukaweka *controls* kwenye maeneo mengine mengi, ukaweka vizuri, lakini hapo ukawa umefeli kwenye jambo moja.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo imekuwa kizungumkuti. Yaani ukisoma mstari kwa mstari kwenye ripoti, utaona kwamba lile lilikuwa shamba la bibi. Hesabu zao zinasema kwamba benki wana pesa, *CAG* anakwenda anakuta pesa kule hakuna. Shilingi bilioni kumi zimeliwa na watu wachache tu, hata sita hawafiki; sijui sita! Shilingi bilioni kumi zimeliwa. Sasa tunasema mapendekezo ya *CAG* yaweze kufanyikwa kazi, ikiwepo waliohusika kuchukuliwa hatua, kwa sababu hiyo ni Taasisi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoielezwa mwanzo, mwanzo ilionekana kama siyo Taasisi ya Serikali lakini ni Taasisi ya Serikali. Naona kengele inagonga, lakini suala la *TRA* pia, wanafanya kazi nzuri, wanafanya kazi kubwa na lazima wasaidiwe. Watasaidiwa vipi kama zile *TRAB* na *TRATH* hazifanyi kazi? Kwa hiyo, ni suala la kuteua; wale Wajumbe wanaohusika wakakaa, mashauri yale yakaisha. Kodi zilizoshikwa kwenye Mahakama za Rufani ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, pia mimi nimefanya kazi *TRA*, uzoefu unaonesha, njia rahisi ya kukwepa au kuchelewesha kukusanya kodi, maana kodi inakusanywa inapokuwa juu. Muda wa kodi ukifika lazima ilipwe. Mtu akiona sasa hapa muda umefika, anakimbilia Mahakamani. Akienda Mahakamani anajificha kwenye mgongo wa sheria, ambapo Bunge ndiyo limetunga hiyo sheria. *One third* inakusanywa au anakwenda kule anakaa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna *tax amnesty* imetolewa hapa, lakini inaonekana bado kuna pesa nyingi zimefungwa kule mashauri hayo hayajamilika. Wale hawatoki kule kwa sababu ndiko walikojificha. Pesa hizi zinazozungumzwa, shilingi bilioni 84 zingeweza kuisaidia sana Serikali hii kuleta matokeo ya maendeleo. Miradi mikubwa inafanyika sasa hivi, hizi pesa zingeweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, *tax arrears* na zenyewe, shilingi bilioni 300 zingeweza kukusanywa nazo zingeweza kusaidia. Ukitafuta sababu, utakuta ni sababu ambazo hawa *TRA* pamoja na kuwa tunawapa *instrument* ya kukusanya kodi lakini bado hawapati msukumo au msaada kutoka kwenye vyombo vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo jambo na lenyewe ni muhimu sana ambalo linatakiwa liangaliwe kwa karibu sana na *TRA* iweze kusaidiwa. Tumeona wamekuwanya zaidi ya asilimia 80. Kukusanya kodi kwa asilimia 80 ni kazi kubwa sana, kwa sababu malengo yanayowekwa ni makubwa. Natambua kabisa, *TRA* wanafanya *revenue forecasting* wanapeleka Hazina. Wakipeleka Hazina kunakuwa na mashauriano kati ya *TRA* na Hazina. Mara zote; hata mimi nilipokuwa *TRA*, Hazina walikuwa wanaweka lengo la juu kwa sababu walikuwa wanataka waji-*stretch* ili Mamlaka iweze kukusanya pesa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiambiwa wamekusanya asilimia 80 ni makusanyo ya kiwango cha juu. Tumeona wanakusanya, sasa wametoka wamekwenda mpaka shilingi trilioni 1.8. Kwa hiyo, hicho ni kiwango kikubwa sana. Lazima sasa na Bunge litoe maazimio ya kuweza kuisaidia *TRA* ili iweze kutekeleza majukumu yake, ikiwepo mambo mengine ya kusaidia watumishi kuweza kuwepo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mzinga. Sasa Mzinga ile na yenyewe imekaa kiaina. Maana yake kuna Shirika Tanzu halafu kuna Ofisi ya Mzinga. Sasa pale mali za Mzinga ndiyo mali za Shirika Tanzu. Hasa hilo na lenyewe lisaidiwe na linafanya kazi kwa hasara. Azimio tuliloliweka huku kwenye Kamati ni jambo la muhimu sana ambalo likichukuliwa na likafanyiwa kazi, tutaiwezesha Mzinga kuweza kufanya kazi zake vizuri na kwa faida na pia iwe na Wakurugenzi wake na iweze pia kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, madeni ya *TANESCO* tumekuwa tukizungumza mara zote; tumeona kuna deni ambalo Serikali

inadaiwa, lakini kuna madeni mengine ya *TANESCO*. Kamati inaendelea kusisitiza na kusihhi Taasisi zinazodaiwa na Wizara zinazodaiwa kuilipa *TANESCO*. Maana tusiwe tunaihukumu *TANESCO* tu kwamba haifanyi vizuri kwenye makusanyo, lakini pesa hizo sisi wenyewe ndio tumekaa nazo. Sisi wenyewe ndio hatulipi pesa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ndiyo ulikuwa huo. Naunga mkono hoja, lakini niseme kwamba nashukuru kwa kuniweka kwenye Kamati hii, nimeweza kuhudumu, nami nimejifunza mambo mengi sana ndani ya Kamati, nikushukuru sana. Ulibadilisha badilisha Kamati lakini hukuweza kunibadilisha, uliniacha hapa hapa. Nakushukuru kwa kuwa nilijifunza mambo mengi, nasi ndio mchango wetu ambao umetupa dhamana kuwa kwenye Kamati ya Mahesabu ya Serikali kama sehemu ya Bunge. Mara zote tumekuwa tukishauri kwa nia ya dhati kuisaidia Serikali na kuona pesa za Serikali hazipotei na mambo yanayopitishwa ndani ya Bunge yanatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa hatua anazozichukua, tunakwenda kufungua shule. Tumuunge mkono, tumtie moyo sisi kama mhimili wa Bunge. Tusiwe tunamvunja moyo, tukimtia moyo, basi na nchi yetu itapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Allan Kiula kwa kutufanyia mapitio ya kazi za Kamati. Kwa kweli Kamati imefanya kazi kubwa sana, tunawashukuruni sana. Keshokutwa Jumanne tutaainisha vizuri na kuwashukuruni rasmi zaidi.

Mheshimiwa Rhoda Kunchela, atafuatiwa na Mheshimiwa Aeshi Hilary ambaye atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo. Mheshimiwa Rhoda.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu

kusimama mbele ya Bunge lako tukufu lakini kabla ya yote nakuomba radhi kwa usumbufu ambao ulijitokeza baada ya kuongea kauli ya kumhusu Mzee wetu, Mheshimiwa Mkono, sikuwa nimetambua kwamba ana hali mbaya kiasi hicho, lakini pia kwa familia yake pamoja na wapiga kura wake.

Mheshimiwa Spika, nijikite sasa na kuendelea katika mchango wangu. Nami pia ni Mjumbe wa Kamati, niongelee mambo machache mawili; kuhusiana na suala la *NIDA*, kama Kamati tumepitia kwenye Taarifa ya *CAG*, kama ambavyo unaelewa kwamba Kamati yetu imekuwa ikisimamia masuala ya fedha, lakini pia inajikita kuangalia na kukagua maeneo ambayo yana ubadhirifu wa pesa na matumizi mabaya kodi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kabisa umuhimu wa *NIDA* pamoja na vitambulisho kwa Watanzania wetu. Ukisoma taarifa ya *CAG* kuna hasara kubwa zaidi ya shilingi bilioni 42 ambayo hawa *NIDA* waliagiza malighafi zaidi, walifanya *overstocking* ya vifaa au malighafi ambazo wao wenyewe walishindwa kuzihifadhi na pia walishindwa kuzitumia kwa sababu waliagiza zaidi kuliko matumizi ya vitambulisho vyenyewe.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kutokuwepo kati ya mkataba wa *NIDA* pamoja na watumiaji. Kwa hiyo, jambo hili pia limesababisha kuikosesha Serikali mapato na Watanzania wetu kuendelea kuhangaika na changamoto ya vitambulisho vya *NIDA* ambapo nchi nzima Watanzania wanahangaika na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali kuhakikisha kwamba inasimamia na ikiwezekana *CAG* aweze kufanya *Special Audit* kwenye haya maeneo kwa sababu kwa kutokuwa na mikataba husika na kwa upotevu wa hizi shilingi bilioni 42 bado kuna haja ya Serikali kuhakikisha kwamba inazifuatilia hizi fedha kwa sababu ni kodi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo suala *TTCL* ambao Wajumbe wengi wameliongelea. *TTCL* imekuwa na upungufu na vituko vingi vya ajabu. Wao wenyewe wanasema wanamiliki Mkongo wa Taifa; Wajumbe wengi wameongelea hapa, lakini ni jambo la aibu sana kwa Shirika kama *TTCL* ambalo linamiliki Mkongo wa Taifa lakini linawauzia *Tigo*. Ukingalia kwenye taarifa za hizi *Market Share*, *TTCL* wana asilimia moja na *Vodacom* wana asilimia 33; wamiliki wa Mkongo wa Taifa, *Airtel* wana asilimia 26, Halotel asilimia 10, *Tigo* asilimia 27. Kwa hiyo, unaweza ukaona kabisa kwamba *TTCL* haiko *serious*.

Mheshimiwa Spika, kuna kituko kingine ambacho *TTCL* wanasema wao wananunua bando wa shilingi 2,500/= lakini wanawauzia wateja kwa shilingi 1,500/=. Kwa hiyo, unaona kwamba *TTCL* haikp *serious* na inafanya biashara ya hasara tangu mwanzo. Wanunua bando wa shilingi 2,500/=: unauza kwa shilingi 1,500/= kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna upungufu ambao nashauri kama Mjumbe wa Kamati; na upo upungufu mwingi ambao Serikali inatakiwa iangalie *TTCL* kwa sababu hata hoja ambazo zimeletwa na *CAG* kwamba walikataa kukaguliwa na walikataa kusaini *report* mbalimbali, hii inaonyesha kabisa ni udhaifu ambao bila kuweka mkazo Serikali inatakiwa iangalie kwa makini ili kuokoa fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pia kuna changamoto za utunzaji wa nyaraka mbalimbali za Serikali, sote tunalewa, tumekuwa tukipitia taarifa mbalimbali za Serikali unakuta nyaraka muhimu za manunuzi ya fedha nyingi zinakuwa hazipo. Kwa hiyo, naomba kabisa hizi *special audit* zinazofanyika na Wakaguzi wa Ndani na wa Nje kuhakikisha hii mfumo inaboreshwa na Serikali iangalie namna gani ya kutunza fedha na hii mifumo ikawa wazi kwa watumiaji na Serikali yenyewe ili kuwa na uwazi wa matumizi haya ya fedha kuanzia kwenye mifumo na taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile yapo mengi ambayo tumeona taasisi mbalimbali za Serikali za 269 ambazo *CAG*

amekuwa akizisimia na amekuwa akikagua matumizi ya fedha pamoja na ubadhirifu ambao unaendelea kwenye hizi taasisi, bado kuna changamoto kubwa tunaiona ya madeni ambayo yanaendelea katika hizi taasisi. Naomba tu hizi taasisi ziweze kulipa madeni. Kuna deni zaidi ya shilingi bilioni 11 ambalo Wajumbe wengi wamesema hapa. *TTCL* ukisoma kwenye taarifa yake wanasema wana zaidi ya shilingi bilioni 11, lakini ukisoma hili deni halionyeshi ni nani anadaiwa, hakuna majina, hakuna matumizi yoyote yanayoonyesha kwamba hili deni ni nani anatakiwa kulilipa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mazingira kama hayo naiomba Serikali yako ya Chama cha Mapinduzi ambayo katika hizi taasisi imeshindwa kusimamia, naweza kusema kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imeshindwa kusimamia kodi za Watanzania. Kwa hiyo, kama ina uwezo ingeweza kuwajibisha taasisi hizi ili tulinde fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru na niunge mkono haja za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aeshi Hilary mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii kuchangia kuwa mchangiaji wa mwisho leo. Naomba nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kuwa Kiongozi mahili na hatimaye sasa tunaelekea mwisho, umri wa muda wetu ni miaka mitano, tunamaliza.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwanza kwa kuniamini na kuiamini Kamati yetu kwa muda wa miaka mitano kufanya kazi na kuhakikisha kwamba tumejisimamia kwa misingi, kwa uzalendo na kuhakikisha kwamba mambo yote yanakwenda vizuri. Naomba nikushukuru sana, sana. Ninaamini kwenye uongozi yapo mambo mengi ambayo yamepita, lakini umekuwa imara

kuhakikisha yale uliyokuwa ukiyapokea unayachuja na hatimaye uyafanyia kazi, nasi kutupa nguvu kama Kamati kufanya kazi kama Kamati kwa uzalendo na kwa weledi mkubwa na hatimaye tunamaliza miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri, Serikali yetu inafanya kazi kubwa sana. Kwa sababu tulipoanza mwaka 2015/2016 tulikuja na hesabu mbaya sana humu ndani, lakini muda ulivyoziidi kwenda Serikali ilichukua hatua kubwa sana. Kwa hiyo, utaona jinsi tunavyokweda *trend* hii, mwaka 2016, 2017, 2018, 2019, 2020, Serikali imefanya kazi kubwa sana ukiangalia na hesabu tulizokuwa tukizileta ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua kubwa anazochukua na pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kuna mambo ambayo tulikuwa tukijadili kwenye Kamati, akiyasikia tu, hatua zimeshachukuliwa. Kwa hiyo, utaona kuna mambo mengi yaliyopita nyuma yameshachukuliwa hatua kali na mambo mengine yamesharekebishika. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa na hatimaye leo tumekuja na taarifa hii na Wajumbe wameweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nilisoma Taarifa ya Kamati, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati yangu. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana. Tumekaa miaka mitano; ni Kamati ambayo ina vishawishi vingi, lakini imesimama imara toka mwaka 2015 mpaka leo hujawahi kusikia kashfa yoyote ile ya Kamati na hatimaye leo hii tunamaliza salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumeshirikiana, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wetu ambaye alikuwa akituongeza kwa muda huu wa miaka mitano, japakuwa kwenye jamii lazima kuna msugvano ya hapa na pale lakini amekuwa akituongeoza vizuri na hatimaye tunamaliza muda wetu. Naomba niwatakie kila la

heri kule mwendako ili muweze kurudi tena ndani ya Bunge hili kuweza kuwatumikia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaongelea jambo moja tu ambalo nimeona kama Mheshimiwa Rhoda hakuliongelea vizuri. Siyo kwamba kuna fedha zimetumika au zimepotea kwa ajili ya kununua vitambulisho au vifaa vya *NIDA*. Kilichotokea *NIDA* ni kwamba mwanzo waliingia Mkataba na Kampuni ya kutengeneza vitambulisho vya Taifa. Tumekwenda baadaye *NIDA* wakaamua kuagiza mitambo mingine mipya. Baada ya kuagiza hii mitambo mingine mipya, kwa nini tunasema tunapata hasara ya shilingi bilioni 42, ni kwamba mitambo iliyokuja na vifaa vilivyokuwepo mwanzo haviingiliani, havisomi pamoja. Kwa hiyo, utaona *stock* walionayo *NIDA* yenye thamani ya shilingi bilioni 42 haitatumika kwa mitambo iliyoingizwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hapo Kamati inasema na *CAG* anashauri, wakati wa kwenda kununua ilitakiwa wazingatie masuala haya kwamba tunapokwenda kununua mitambo hii tuhakikishe kwamba mwanzo tulikuwa tunatengeneza vitambulisho vingine vya Taifa. Kwa hiyo, kungekuwa na mwingiliano wa masuala haya ya *system* ambayo yamekuja kuwekwa ambayo ni mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuzingatia hivyo, Serikali au *NIDA* wataingia hasara ya shilingi bilioni 42 ambayo ni *stock* iko ya vitambulisho ambavyo havijatumika. Kwa hapo ndiyo kuna kosa na Kamati imeliona na *CAG* alishauri kwamba utaratibu huu haukufuatwa.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, wakati wanatangaza kwamba sasa tununue vifaa vingine, hawakufuta utaratibu. Kwa hiyo, suala hili ndiyo utaliona, laiti wangufuata utaratibu wa *tender*, wangetangaza na watu wakajitokeza, labda ingeweza kuokoa fedha hizi. Kwa hiyo, fedha hizi zilitumika kununua vitambulisho na vipo. Siyo kwamba ni fedha labda zimeibiwa au zimepotea, hapana, vitambulivyo vipo isipokuwa havitaweza kutumika vyenye thamani ya shilingi bilioni 42.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nilitoa hoja, naomba Jumanne wakati nakuja hapa ku-*wind* up tutajibu mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana, Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Kama mnavyojua, tutaendelea na mjadala huu siku ya Jumanne *Inshallah*. Tumeona tumalizie hapa kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wamenitaarifu kwamba jioni ya leo baadhi watakuwa wanasafiri kwenda maeneo mbalimbali ya nchi ili kujiunga na familia zao kwa ajili ya Siku Kuu ya Idd. Kwa hiyo, nami nichukue nafasi hii kuwatakia kila la heri Waheshimiwa Wabunge wote na familia zenu popote pale zilipo, nitangulize salamu za Idd Mubarak. (*Makofi*)

Basi tukumbukane katika sala na dua za siku hiyo na niwatakie kila la heri katika Mwezi Mtukufu, kumalizia mfungo; naamini kabisa tutamaliza salama. Kwa hiyo, kwa kuwa Idd inategemeana na mwandamo, tunakadiria kwamba huenda ikawa Jumapili au Jumatatu, lakini ikitokea tofauti na hapo, basi tutarekebisha ratiba yetu *accordingly*, kwamba hapa tutakapoahirisha, tunaahirisha hadi siku ya Jumanne, lakini ikitokea; hatuna hakika kwamba Jumanne ni Idd Pili, basi tutakutana Jumatano. Kwa hiyo, hapo tuelewane vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha, basi nitoe tangazo moja kwa Waheshimiwa Wabunge. Nilipokea ombi na nikalikubali la kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali, Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed la kutoa sadaka ya mchele kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi kuanzia leo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho yake yeye na sadaka katika Mfungo huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Naomba kwa niaba yenu nimshukuru sana Mheshimiwa Haroon kwa sadaka hiyo kwa niaba yenu nyote. Mchele huo umeanza kugaiwa katika eneo la *basement*

hapo chini kuanzia leo, kwa hiyo, kila mmoja kwa wakati wake anaweza kupitia mchele huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haroon amekuwa akitoa sadaka hii *almost* kila mwaka kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge. Kwa kweli tunamshukuru sana, yeye ni mkulima wa mpunga, kwa hiyo, anatoa kama sehemu ya mazao kutoka shambani. Kwa hiyo, kila mmoja ukipa nafasi basi pitia kwa sababu itakapofika kwenye Jumanne huko na Siku Kuu ikawa imeshapita, basi utakuta Watumishi wa Bunge wameshagawiana. Kwa hiyo, msisahau kupitia mchele huo tafadhali, mpelekee familia.

Basi Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza tutaendelea na mjadala wetu siku Jumanne. Naomba nichukue fursa hii sasa kuahirisha Shughuli za Bunge hadi siku ya Jumanne wiki ijayo au kama nilivyowaeleza kutegemeana na Sherehe za Idd zitakavyokuwa. Ahsante sana.

(Saa 10.23 jioni Bunge liliarishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 26 Mei, 2020, Saa Nane Kamili Mchana)